# Nipashe

Jumatano Septemba 2, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580326

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## CHADEMA yaanika mambo 16 siku 100 za mwanzo Ikulu

UKURASA 3




UKURASA 11

# Mwendo wa ahadi

• **JPM** asema umeme vijiji vyote miaka miwili ijayo, ACT-Wazalendo yaahidi uchumi wenye tija, Lissu atamba kuleta neema ... *Endelea ukurasa 2, 4*



Mgombea urais kupitia CCM, Rais John Magufuli, akizungumza na wananchi wa Mkoa wa Singida kwenye mkutano wa kampeni katika uwanja wa Bombardier, mjini Singida jana. **PICHA: IKULU**



Mgombea urais kwa tiketi ya ACT-Wazalendo, Bernard Membe, akihutubia wakati wa uzinduzi wa kampeni, mjini Lindi jana. **PICHA: ENOCK CHARLES**



Mgombea urais kupitia CHADEMA, Tundu Lissu, akihutubia mkutano wa kampeni katika viwanja vya Furahisha, jijini Mwanza jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Kizimbani tuhuma za mauaji ya kada CCM

UKURASA 3



## Mapingamizi 557 yatua NEC

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu



**MICHEZO** SIMBA YAPELEKA SHANGWE MBEYA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# JPM: Vijiji vyote kupata umeme mwaka 2022

**Na Gwamaka Alipipi, SINGIDA**



MGOMBEA urais kupitia tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais John Magufuli, amesema ifikapo mwaka 2022 atahakikisha vijiji vyote nchini vinafikiwa na umeme.

Amesema wakati anaingia madarakani mwaka 2015, idadi ya vijiji vilivyokuwa na umeme nchini vilikuwa 2,018, na kuwa kwamba hadi mwaka huu idadi hiyo imeongezeka na kufikia vijiji 9,570, huku vikisalia vijiji 2,600.

Alitoa ahadi hiyo jana katika uwanja wa Bombadier mkoani Singida, wakati akiwahutubia wananchi waliojitokeza kumsikiliza wakati akiomba ridhaa ya kuchaguliwa tena kuliongoza Taifa kwa miaka mingine mitano.

"Ninawahakikishia Watanzania kwamba ndani ya miaka miwili baada ya kuingia madarakani vijiji vyote nchini vitakuwa vimefikiwa na huduma ya umeme, kama tumeweza kufikia vijiji zaidi ya 7,000 vitanishindaje vijiji 2,600 vilivyobakia, kwa sababu idadi ya vijiji vyote nchini ni 12,280," alisema na kuongeza:

"Nadhani mnakumbuka kulikuwa na mgawo wa umeme nchini, lakini sasa imebaki historia, sasa nipeni tena miaka mitano nikahakikishe nchi nzima kunakuwa na umeme, ninaomba kura kwa wananchi wa vyama vyote kwa sababu maendeleo hayana chama."

### WAKULIMA KUTAFUTIWA MASOKO

Mbali na kuahidi kutekeleza hilo, pia aliwahakikishia Watanzaia hususani wakulima kwamba watawekewa utaratibu mzuri wa kuhakikisha wanauza mazao yao vizuri pamoja na kutafutiwa masoko.

Akizungumzia kuhusu ujenzi wa viwanda, Rais Magufuli alisema: "Miaka mitano ijayo tutaendelea kujenga viwanda vingi zaidi, hadi sasa idadi ya viwanda nchini vimefika 61,000."

Alisema serikali yake katika kipindi cha miaka mitano ijayo imetengeneza ajira zaidi ya milioni sita, kwamba miaka mitano ijayo ajira zaidi ya milioni nane zitatengenezwa.

Kuhusu mkoa wa Singida, alisema katika kipindi cha miaka mitano miradi ya maji 66 yenye thamani ya Sh. bilioni 27.2 imetekelezwa sambamba na uchimbaji wa visima vinne virefu vya maji.

Aidha, alisema zaidi ya Sh. bilioni 470.4 zimetumika katika kipindi cha miaka mitano kwenye mkoa huo kwa ajili ya utekelezaji wa miundombinu ya kiuchumi, kati ya fedha hizo Sh. bilioni 95.3 zilitumika katika miradi ya umeme na Sh. bilioni 213 katika ujenzi wa barabara, madaraja na karakana.

"Tumejenga barabara ya Manyoni-Itigi kwa kiwango cha lami, barabara kuanzia Chaya-Tabora yenye urefu wa kilometa 85 imejengwa kwa kiwango cha lami sambamba na ujenzi wa daraja la Sibiti. Pia tumetumia Sh. bilioni 17 kujenga barabara kuanzia Karume-Boma-Kinyeto," alisema Rais Magufuli.

Pia Serikali katika kipindi cha miaka mitano imejenga barabara kuanzia mkoani Singida hadi Babati, Singida hadi Mwanza.

### AMANI KULINDWA

Awali akiwa wilayani Bahi, Rais John Magufuli alisema atahakikisha anaendelea kulinda na kudumisha amani iliyopo nchini wakati wote.

Alisema Tanzania ni sehemu yenye usalama zaidi Afrika na duniani, hivyo atahakikisha usalama huo unaendelea kuwapo wakati wote.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na umati wa wananchi waliojitokeza katika Uwanja wa Shule ya Msingi Sokoni.

"Kwa mujibu wa takwimu za Taasisi ya Global Peace Index ya mwaka 2020, Tanzania tunashika nafasi ya kwanza kwa nchi za Afrika Mashariki zenye usalama zaidi, nafasi ya sita kwa nchi za Afrika na nafasi ya 52 duniani, hivyo wananchi wa Bahi nawaomba tuendeleze amani hii," alisema Rais Magufuli.

Aliwaahidi wakazi wa Bahi mambo makubwa sita, ikiwamo kumaliza kero sugu ya upatikanaji wa maji, huduma bora za afya na kuboresha sekta ya elimu.

"Nitawaletea maji, hivi sasa tumeanza upembuzi yakinifu wa mradi wa maji wa Ibimwa..mimi ninakaa Chamwino Dodoma, kutoka ninapokaa hadi Bahi ni pua na mdomo, hivyo sitashindwa kuwaletea maji, ninachotaka ni kura zenu tu," alisema Rais Magufuli.

Alisema endapo akiingia madarakani, atahakikisha shule za msingi na sekondari zinajengwa katika wilaya hiyo, kuboresha elimu bure ili kuwawezesha watoto waweze kusoma vizuri.

Alisema pia atahakikisha idadi ya walimu katika shule za Wilaya ya Bahi wanaajiriwa kwa wingi ili kuendana na idadi ya shule na wanafunzi.

Rais Magufuli aliwaahidi wakazi hao kuwatatulia huduma ya maji, ambayo imekuwa ikiwatesa kwa muda mrefu kwa kujenga miradi ya maji na uchimbaji wa visima.

Alisema zaidi ya Sh. bilioni 2.9 zimeshatengwa katika kutatua kero hiyo kwamba mradi wa maji wa Mdemu, Mgaga imeshajengwa.

Alisema akiingia madarakani atahakikisha skimu ya umwagiliaji inajengwa ili kuwawezesha wakulima wa mpunga kulima kwa ufanisi, sambamba na wafugaji waweze kunywesha mifugo yao.

Alisema miaka mitano ijayo atahakikisha Wilaya ya Bahi inajengwa miundombinu iliyo bora ikiwamo ujenzi wa barabara za lami.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano ya utawala wake amejenga vituo vya afya vitatu kwa gharama ya Sh.bilioni 1.5, na sasa hivi kunajengwa hospitali ya wilaya ambayo ujenzi wake umeshakamilika kwa asilimia 95 kwa gharama ya Sh. bilioni 1.8.

Kadhalika, alisema katika kipindi cha miaka mitano ya utawala wake Wilaya ya Bahi ilipata Sh.bilioni 5.7 kwa ajili ya kaya masikini, Sh.milioni 149 kwa ajili ya kuwapatia mikopo wanawake, vijana.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
KANDA YA MTWARA

SHAURI LA ARDHI NA. 4/2018

(Asilia Shauri la Madai ya Ardhi Na. 4/2018,Mahakama ya Ardhi Mtwara)

AUGUTA LEO HENJEWELE.......................................................................................MRUFANI

DHIDI YA

HAMISI JUMA NCHII NA WENZAKE (127)...........................................MJIBU RUFAA

KUITWA SHAURINI

KWA:
HAMISI JUMA NCHII NA WENZAKE (127)
CHIPUTA MAGOMENI
MTWARA

HII NI KUWATAARIFU KUWA MNAAMRIWA KUFIKA MBELE YA MAHAKAMA KUU MTWARA KUSIKILIZA SHAURI HILI MNAMO TAREHE 24/09/2020 SAA 2:30 ASUBUHI BILA KUKOSA.
KUMBUKA KUWA ENDAPO HAMTAFIKA NYIE WENYEWE AU MTU YEYOTE ANAYERUHUSIWA KISHERIA KUWAWAKILISHA, BASI SHAURI HILI LITASIKILIZWA NA KUAMRIWA BILA NINYI KUWEPO.
IMETOLEWA KWA AMRI YANGU NA KWA MHURI WA MAHAKAMA LEO HII TAREHE 28/07/2020.

A.H. MSUMI
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MTWARA

215882302


## Rufani 557 zatua NEC

**Na Halfani Chusi**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imepokea rufani 557 kutoka kwa wagombea wa nafasi za ubunge na udiwani ambao hawakuridhishwa na uamuzi wa wasimamizi wa uchaguzi.

Mwenyekiti wa tume hiyo, Jaji mstaafu Semistocles Kaijage, aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salam jana kuwa walianza kuzifanyia kazi rufani hizo jana na wamejipanga kuhakikisha uamuzi unatolewa mapema kwa kadri itakavyowezekana.

Alisema rufani hizo zinashughulikia kwa mujibu wa sheria za uchaguzi na kanuni zake zilizoweka masharti, taratibu na hatua za kuchukua panapokuwa na malalamiko au ukiukwaji wa sheria na taratibu za uchaguzi.

Kiongozi huyo wa tume pia aliwapongeza wagombea wa vyama vya siasa ambao wamefuata taratibu sahihi kudai haki zao kwa kuwasilisha rufani kwa tume baada ya kutoridhishwa na wasimamizi wa uchaguzi huo.

Jaji Kaijage alisema taratibu zimebainishwa katika hatua mbalimbali za uchaguzi kuanzia uteuzi wa wagombea hadi kutangaza matokeo, hivyo ni wajibu wa vyama vya siasa kujua haki zao na hatua za kuchukua kwa mamlaka husika pale panapotokea kutoridhika na jambo kipindi chote cha uchaguzi.

"Tunavipongeza vyama vya siasa ambavyo vimeanza kampeni zake, lakini pia nivikumbushe vyama vya siasa na wagombea kufanya kampeni za kistaarabu zinazozingatia maadili ya uchaguzi. Maadili hayo wahusika wake wakuu ni serikali, NEC, vyama vya siasa na wagombea.

"Hatutarajii kuona vyama vya siasa vikilalamika kuhusu ukiukwaji wa maadili ya uchaguzi, badala ya kuchukua hatua stahiki kisheria kwa mamlaka husika. Hatua hizo ni pamoja na kuzitumika kamati za maadili ambazo zimepewa mamlaka ya kushughulikia malalamiko yanayohusu ukiukwaji wa maadili ya uchaguzi," alisema.

Jaji Kaijage aliwataka wadau wote, wakiwamo waandishi wa habari, kuendelea kusoma kitabu cha maelekezo ya vyama vya siasa na wagombea wa mwaka 2020 ambacho kina ufafanuzi wa mchakato wote wa uchaguzi kuanzia uteuzi wa wagombea, mapingamizi, rufani, kampeni na maadili, mawakala wa vyama vya siasa na hatua za upigaji kura hadi kutangaza matokeo.

# Kortini tuhuma mauaji kada CCM

**Na Thobias Mwanakatwe**

WATU 16 wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Mkoa wa Songwe juzi, wakikabiliwa na shtaka la mauaji ya anayedaiwa kuwa ni kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Briton Mollel.

Mauaji hayo yalitokea baada ya kuzuka vurugu kati ya watu wanaodaiwa kuwa wafuasi wa CCM na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na kusababisha watu wengine wawili kujeruhiwa.

Waliofikishwa mahakamani ni Peter Charahani, Ijumeleghe Mwanjila, Elia Sichone, Charles Simkonda, Daudi Mwajunga, Wiliam Simkoko, Oscar Philip, Yohana Mkumbwa, Feston Kitta, Tonny Siwale na Ayubu Mwakasege.

Wengine ni James Simkoko, Julius Wilson, Emmanuel Msinjili, Hidaya Mwangoka na Jenifer Mwasenga.

Wakili wa Serikali, Renatus Mkude, alidai mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Kassim Mkwawa, kuwa watuhumiwa walitenda kosa hilo Agosti 25, mwaka huu katika eneo la kata ya Mwakakati Mji wa Tunduma wilayani Momba, mkoani Songwe.

Akiwasomea shtaka hilo katika kesi hiyo ya jinai namba 196 na 1997, Wakili Mkude alidai kuwa washtakiwa kwa pamoja walitenda kosa hilo la kuua kinyume cha kanuni ya adhabu Sura ya 16 ya Sheria za Tanzania.

Aliendelea kudai kuwa washtakiwa pia wanakabiliwa na kosa la kuwajeruhi kwa mapanga Francis Simumba na Elisha Sifa kinyume na Kifungu cha 22(a) cha kanuni ya adhabu sura ya 16 ya Sheria za Tanzania.

"Kosa lililofanywa na washtakiwa 16 ni kubwa sana, kwani kuua na kukatisha maisha ya binadamu ni kosa la jinai ambalo ni kinyume cha kanuni ya adhabu sura ya 16 ya Sheria za Tanzania," alidai Mkude.

Hakumu Mkwawa aliiahirisha kesi hiyo hadi Septemba 14, mwaka huu, ambapo watuhumiwa walirudishwa mahabusu kwa sababu kesi hiyo haina dhamana.

**Kosa lililofanywa na washtakiwa 16 ni kubwa sana, kwani kuua na kukatisha maisha ya binadamu ni kosa la jinai ambalo ni kinyume cha kanuni ya adhabu sura ya 16 ya Sheria za Tanzania.**

# CHADEMA yataja mambo 16 siku 100 za kwanza ikishinda

**Na Salome Kitomari**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimeainisha mambo 16 kitakachofanya siku 100 za kwanza iwapo kitachaguliwa na kupewa ridhaa ya kushika dola katika uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani utakaofanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Katika Ilani yake yenye kurasa 104, chama hicho kimetaja mambo 16 ya kipaumbele ambayo yatatekelezwa siku 100 za kwanza, ambayo pamoja na mambo mengine itapeleka bungeni muswada wa sheria mbalimbali ikiwamo ya maridhiano.

Pia, ilani hiyo imeainisha vipaumbele 20 katika kujenga nchi yenye demokrasia, utawala bora na haki za binadamu.

Ilani hiyo imebainisha kuwa serikali ya CHADEMA itapeleka bungeni muswada wa sheria ya maridhiano ambayo pamoja na mambo mengine, itaanzisha Tume ya Maridhiano kwa lengo la kuondoa hofu ya uwezekano wa vitendo vya kulipiza visasi na kuunganisha nguvu za wananchi wote bila ubaguzi wa vyama katika kuongoza taifa.

### FAO LA KUJITOA

Pia imejinasibu kuwa ndani ya siku hizo itapeleka bungeni muswada wa marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Jamii ili kurekebisha kikokotoo cha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa wastaafu ili kiendane na mahitaji ya wastaafu.

"Serikali ya CHADEMA itaruhusu wafanyakazi na watumishi waliochangia katika mifuko ya jamii kuchukua mafao yao wakati wowote (Fao la kujitoa)," ilisema.

### UBIA SEKTA BINAFSI

Ilani hiyo imebainisha kuwa itapeleka muswada wa sheria ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi juu ya utoaji wa elimu bure kuanzia elimu ya awali hadi sekondari.

### MIKOPO ELIMU YA JUU

Aidha, imesema itapunguza kiwango cha marejesho ya mikopo ya elimu ya juu hadi kufikia asilimia tatu ya mshahara wa mnufaika na kutanua wigo wa muda wa marejesho hadi kufikia miaka 25 tangu mnufaika apate ajira.

Kadhalika, imesema itafuta riba na tozo zote zitokanazo na adhabu ya kuchelewesha marejesho ya mkopo wa elimu ya juu.

### AFYA IMARA

"Serikali ya CHADEMA itashirikiana na sekta binafsi kuweka utaratibu wa kutoa huduma za afya ya msingi kwa wananchi bila malipo," ilisema sehemu ya ilani hiyo.

### KATIBA MPYA

Kwa mujibu wa ilani hiyo, serikali hiyo itarejesha mchakato wa Katiba Mpya kuanzia iliyoishia Rasimu ya Tume ya Marekebisho ya Katiba ya Jaji Warioba.

Aidha, Serikali ya CHADEMA itatekeleza matakwa ya Katiba kuhusu Tume ya Pamoja ya Fedha ya Muungano ili kila nchi mshirika wa Muungano ipate mgawo wake wa fedha kwa mujibu wa Katiba na sheria.

### UHURU WA HABARI

Pia CHADEMA imejinasibu kuwa itarejesha uhuru wa vyombo vya habari ikiwa ni pamoja na kuruhusu kurushwa moja kwa moja vikao vya kamati za Bunge, mikutano ya Bunge na mwenendo wa uendeshaji wa mashauri mahakamani.

### SHERIA KANDAMIZI

Chama hicho kimejinasibu kuwa ndani ya siku 100 za kwanza itapeleka miswada ya sheria bungeni kwa madhumuni ya kufuta sheria zote kandamizi na zinazokiuka misingi ya haki za binadamu.

### MUUNGANO

Kwa mujibu wa Ilani hiyo, CHADEMA imesema itaanzisha utaratibu wa mazungumzo kati ya serikali ya Jamuhuri na Zanzibar kwa lengo la kufikia muafaka juu ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi, uvuvi wa bahari kuu na usajili wa meli.

### WALIOCHA SHULE

"Serikali ya CHADEMA itaandaa mazingira rafiki na wezeshi kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari walioshindwa kuendelea na masomo kwa sababu mbalimbali kama vile ugonjwa, kukosa ada, mimba kurejea kwenye mfumo rasmi wa elimu na kuamlizia masomo yao," ilisema sehemu ya ilani hiyo.

### MISHAHARA WATUMISHI

Aidha, ilani hiyo ilibainisha kuwa itapeleka bajeti ya nyongeza bungeni katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kuongeza mishahara ya watumishi wote wa umma, kulipa malimbikizo, sambamba na kuwapandisha madaraja watumishi wenye sifa na kulipa mishahara inayoendana na madaraja yao.

### BIMA MAALUM

Pia imesema itaanzisha bima maalum ya afya kwa watumishi wote wa vyombo vya ulinzi na usalama wawapo kazini na baada ya kustaafu vikiwamo Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Polisi, Magereza, Uhamiaji, Zimamoto na Uokoaji.

### MADUKA YA JESHI

CHADEMA imesema itarejesha maduka yasiyotozwa kodi katika vyombo vya ulinzi na usalama vikiwamo Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Polisi, Magereza, Uhamiaji, Zimamoto na Uokoaji.

### MASOKO YA BIDHAA

Aidha, ilani hiyo ilibainisha kuwa itaweka utaratibu na kuwatafutia masoko wakulima, wavuvi na wafugaji ya kuuza mazao yao ndani na nje ya nchi bila kizuizi.

Pia, kurejesha utaratibu wa awali wa ukusanyaji wa kodi, ushuru na tozo mbalimbali kwa mamlaka ya serikali za mitaa.


MARCAS
DEBT COLLECTORS AND AUCTIONEERS (T) LTD.

MNADA WA HADHARA

**MARCAS DEBT COLLECTORS & AUCTIONERS LTD,** kwa idhini tuliyopewa na **KCB Bank Tanzania Limited** P.O. Box 804 Dar es Salaam, tutauza nyumba kwa njia ya mnada zilizopo maeneo ya Mikocheni Manispaa ya Kinondoni Dar es Salaam. Tarehe **23 Septemba 2020** Wakaguzi wote mnakaribishwa kukagua nyumba tarehe **22 Septemba 2020** saa 4:00 Asubuhi - 9:00 alasiri.

| NAMBA | ENEO | MUDA |
|---|---|---|
| Plot 489, CT.30063, L.O. 75309 | Mikocheni | 4:00Asubuhi - 9.00 Alasiri |

MASHARTI YA MNADA

1. Mshindi atalipa 25% papohapo baada ya nyundo ya dalali kushuka na kiasi kinachobakia yaani 75% italipwa ndani ya siku 14 baada ya siku ya mnada. Mnunuzi atakayeshindwa kulipa 75% zilizobakia atapoteza ushindi wake na hatarudishiwa kiasi cha awali cha 25% na mali hii itanadiwa tena.
2. Nyumba na viwanja vitauzwa kama zilivyo.
3. Wanunuzi watatakiwa kufika na vitambulisho vyenye picha zao ambavyo vinatambulika na serikali.
4. Mnunuzi atalipa gharama za uhamisho.

215882102

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa simu: 0752722222/0713268383



KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
DAR ES SALAAM

UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI

MIRATHI Na. 56 YA MWAKA 2020

MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU

ALOYCE BENTI KIMARO
MWOMBAJI/WAOMBAJI

OLIVIA ALOYCE KIMARO NA MWENZAKE

TAARIFA YA KAWAIDA
(KANUNI YA 75)

Watu wanaodaiwa kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika Jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa Waombaji/Mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 22 mwezi wa 9,2020

Imewasilishwa Dar es Salaam, leo 31 mwezi wa 08, 2020.

NAIBU MSAJILI

NAIBU WAZIRI
NAKALA KWA:
GODSON HUDSON NYANGE(ADV)
NW LAW ASSOCIATES
HOUSE NO.16 CORNER OF HAILE SELESSIE / GHUBA ROAD
OYSTERBAY
P.O BOX 5049
D'SALAAM.

115881502

# Bernard Membe aahidi nyongeza ya mishahara

**Na Enock Charles, LINDI**



MGOMBEA urais wa Chama cha ACT-Wazalendo, Bernard Membe, ameahidi kuongeza mishahara ya watumishi wa umma na kulipa malimbikizo ya madai yao kwa Serikali atakapochaguliwa Oktoba 28, mwaka huu.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni katika Mkoa wa Lindi jana,Membe alisema kutoongezwa kwa mishahara ya watumishi kunapunguza ufanisi wa kazi.

"Serikali ya ACT -Wazalendo itahakikisha wafanyakazi wanapewa nyongeza yao ya mishahara ya kila mwaka, fedha zao za likizo na malimbikizo ya madeni," alisema Membe.

**AFUNGUKA KUHUSU KOROSHO**

Akizungumzia korosho, Membe alikosoa utaratibu wa kuzuiwa kwa watu wanaojulikana kama 'kangomba' kununua na kuuza korosho za wakulima hasa katika mikoa ya kusini na badala yake korosho kununuliwa na Serikali.

Alisema hatua hiyo imeleta maumivu baada ya baadhi ya wakulima ama kulipwa kidogo au kucheleweshwa kwa fedha zao za korosho, huku pia akitupia lawama kwa Serikali kutokana na kuporomoka kwa bei za mazao ya wakulima yakiwamo mbaazi na ufuta.

"Kumwambia mtu anayekuuzia korosho akuonyeshe shamba kwani wanaouza machungwa na ndizi Dar es Salaam huwa wanaonyesha mashamba?" alihoji Membe.

Pia alikosoa utaratibu wa baadhi ya hospitali kutoza fedha za gharama za matibabu hata kwa mtu aliyefariki, na kuahidi kuboresha huduma za afya hasa suala la bima ili kupunguza makali ya gharama za matibabu, huku wazee,wajawazito na watoto wakiahidiwa huduma bora zaidi.

**ALICHOKISEMA ZITTO**

Awali, Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, alisema katika kipindi cha miaka mitano CCM ilipewa ridhaa ya kuongoza nchi na sasa wana siku 60 za kupimwa kama wana nafasi ya kuendelea kuongeza miaka mingine mitano.

Alisema CCM waliahidi kuwa Tanzania itakuwa nchi ya uchumi wa gesi na mikoa ya Lindi na Mtwara itakuwa vitovu vya gesi, lakini hawajatekeleza.

Zitto alisema Serikali ya awamu ya nne, iliacha mradi mkubwa wa dola bilioni 30, sawa na Sh. trilioni 60 kwa ajili ya maendeleo ya gesi katika mikoa hiyo.

Alisema katika ilani ya uchaguzi ya mwaka 2015/20, CCM waliahidi kuwa Tanzania itakuwa uchumi wa gesi.

"CCM iliahidi katika ilani yake kuwa Tanzania itakuwa nchi ya uchumi wa gesi, watu wa Lindi mmeona uchumi wa gesi, watu ambao hawakutekeleza ahadi yao, mtawachagua tena?" alihoji Zitto.

Alisema kwa miaka mitano, Serikali imeshindwa kutekeleza mradi wa gesi katika mikoa hiyo.

Kadhalika, alidai Serikali ya CCM imeshindwa kukarabati barabara ya Lindi ambayo imekuwa mbovu kwa zaidi ya miaka mitano.

Kuhusu korosho, Zitto alisema limekuwa kilio kwa watu wa kusini na halijatafutiwa ufumbuzi.

Alisema pia ahadi ya Sh. milioni 50 kila kijiji na ajira milioni moja hazijatekelezwa.

Zitto alisema Ilani ya Uchaguzi ya ACT-Wazalendo inaenda kurasimisha biashara ya mazao ili kila mkulima auze mazao yake bila kuwa na changamoto.

## Tiba asili wampa 5 JPM

**Na Beatrice Shayo**

WATAALAMU wa tiba asili wamempongeza Rais John Magufuli kwa kutambua na kuthamini mchango wao kwa wananchi.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa Sauti ya Wataalamu wa tiba asili, Juma Mwaka, wakati akitoa tamko la wataalamu wa tiba asili kwa waandishi wa habari jijini Dar es Salaam.

Alisema kuna baadhi walikuwa wakiwadharau na kuwauliza wataalamu wa tiba asilia, lakini Rais Magufuli hakuliangalia hilo na kuendelea na msimamo wake wa kuthamini huduma wanazozitoa kwa wananchi.

"Tunatoa shukurani zetu kwa Rais Magufuli kwa kutambua na kuthamini mchango wa tiba asilia, na hata kurekebisha sekta ya afya kwa kutoa agizo na mwongozo wa namna ya kutumia tiba asili kama njia sahihi ya kupambana katika kujikinga na ugonjwa wa Covid-19," alisema Mwaka.

Alisema Agosti 29, mwaka huu Rais Magufuli wakati akizindua kampeni jijini Dodoma alieleza kuwa atahakikisha wataalamu wa tiba asili wanatambulika na wao wameahidi kutomwangusha.

Aidha, alisema Rais Magufuli amesaidia kuwatoa hofu wananchi kuhusu utumiaji wa tiba asili, jambo ambalo lisingesimamiwa lingesababisha kutokea athari.

Aidha, alisema hivi karibuni Shirika la Afya Duniani (WHO) imetoa takwimu kuwa asilimia 80 ya watu kutoka mataifa yanayoendelea wanatumia tiba asili, huku Tanzania ikitoa mchango wa zaidi ya asilimia 45 ya kutatua changamoto mbalimbali za kiafya.

Naye Mratibu wa tiba asili Manispaa ya Ilala, Dk. Walter Macha, alimwomba Rais Magufuli na serikali kuwawekea mazingira rafiki ili kutengeneza bidhaa za tiba asili na kuziuza nje ya nchi wapate fedha za kigeni.

fcs
FOUNDATION FOR CIVIL SOCIETY
Facilitating Partnerships for Development

**EXPRESSION OF INTEREST FOR SUPPLY OF ACCOUNTING SOFTWARE (PACKAGE)**

Foundation for Civil Society (FCS) an independent Tanzanian non-for-profit organization providing grants and capacity building services to Civil Society Organizations (CSOs) in Tanzania. Our mission is to contribute to sustainable development in Tanzania through civil society strengthening, policy influencing and enhancing a learning culture.

The FCS invites applications from credible, eligible and well-established service providers to express interest to supply suitable Accounting Software capable of supporting Accounting systems for Non-Government / Non-commercial undertaking.

Short listing criteria will include;

(i) Company Profile and physical location, possession of business licence, tax clearance certificate, certificate of incorporation, business registration, TIN, and VAT Certificate.
(ii) A minimum of two (4) years' experience in the field and recommendation from, at least (4) three customers.
(iii) Documented financial capacity, technical competence and ability to deliver good services.

Applications in plain sealed envelopes, clearly showing the title of the tender "Supply of Accounting Package", should be addressed to:

**Chairperson – FCS Procurement Committee,**
**P.O. Box 7192,**
**7 Madai Crescent, Ada Estate, Plot 154**
**Dar es salaam**

Deadline for submission of Expression of Interest shall be 15th, September 2020 at 16.00 and they will be opened on the same date.

The Foundation for Civil Society is not obliged to accept the lowest or any tender.

**Executive Director**
**Foundation for Civil Society**
**7 Madai Crescent, Ada Estate, plot 154**
**P.O Box 7192, Dar es Salaam. Tel:+25522-2664890-2, Fax: +255 22-2664893**
**E-mail: information@thefoundation.or.tz**

## Lissu atamba kuleta neema

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

MGOMBEA urais wa Tanzania kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), ameahidi neema kwa wakulima, wavuvi, machinga na wafanyakazi ikiwa atafanikiwa kushinda kiti hicho katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu.

Akihutubia maelfu ya wananchi waliojitokeza katika mkutano wake wa uzinduzi wa kampeni za chama hicho Kanda ya Ziwa jijini Mwanza jana, Lissu alisema serikali atakayoiongoza italeta shangwe kwa wakulima, wavuvi, machinga, walimu, manesi na madaktari, huku akiacha maswali ambayo alitaka wananchi wawaulize viongozi wa chama tawala watakapokuwa wanaomba kura mwaka huu.

Lissu ambaye kitaaluma ni mwanasheria, alisema kuwa endapo wakishinda katika uchaguzi huo, serikali yao itahakikisha wakulima wananufaika na mazao yao, akilitolea mfano zao la pamba ambalo kwa Kanda ya Ziwa kwa muda mrefu limekuwa tegemeo kubwa kibiashara.

Alisema serikali yao itahakikisha wakulima wanapata bei nzuri na soko la uhakika na pembejeo kwa wakati.

Lissu alisema serikali yao pia itapiga marufuku wafanyabiashara wadogo, maarufu machinga, kuuziwa vitambulisho vya wajasiriamali na kuwatoa kwenye mitaro kwa kuwajengea majengo makubwa ya kibiashara.

Akifafanua kuhusu ahadi yake hiyo, Lissu alisema kila machinga atakuwa na eneo rafiki kibiashara, akitamba kuwa wafugaji na wafanyabiashara watarajie kuneemeka.

"Agano langu kwa watu wa Mwanza na Kanda ya Ziwa, wavuvi serikali yangu haitataifisha nyavu zenu, bali italinda haki zenu. Na ninyi machinga mnafanya biashara kwenye mitaro. Huo ni udhalilishaji. Nitawatengenezea mazingira mazuri, hivyo mchague CHADEMA.

"Walimu, manesi na madaktari maslahi yenu nitayatetea. Ilani yetu ya uchaguzi inasema uhuru na haki kwani bila huru, wananchi wa Tanzania hawawezi kusema wapo huru bila ya kupata mambo niliyoyataja," alisema.

Akihitimisha mkutano wake huo, Lissu aliwaka wakazi wa Mwanza na Kanda ya Ziwa kuwauliza viongozi wa CCM maswali kadhaa, ikiwamo kuwatajia majina ya watu aliodai wameua viwanda jijini Mwanza na ziliko fedha za malipo ya pamba ya wakulima wa Kanda ya Ziwa.

## Wanafunzi wenye ualbino wasaidiwa kompyuta 91

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Under the Same Sun (UTSS) limewapatia kompyuta mpakato wanafunzi 91 wenye ualbino wanaojiunga na vyuo vikuu na vya kati ili ziwasaidie kurahisisha ufanyaji kazi kutokana na tatizo la uoni hafifu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Meneja Elimu, Mafunzo na Ajira, Grace Wabanhu wakati akikabidhi kompyuta mpakato kwa wanafunzi 18 wa awamu hii, alisema tangu mwaka 2018 wamekuwa wakifanya hivyo.

Alisema ufadhili huo wa kompyuta na mafunzo ulianza mwaka 2018 na umekuwa ukitolewa na Taasisi ya Vivian Grace Ash (mke wa Ofisa Mtendaji Mkuu na mwasisi wa UTSS) pamoja na Open Chapel Society zote za Canada.

"Leo (jana) jumla ya wanafunzi 18 walio kwenye ufadhili wa mafunzo awamu hii wamepatiwa kompyuta mpakato na wananufaika na mafunzo ya siku 25 yaliyoanza Agosti 26. Tangu tuanze tumeshatoa kwa wanafunzi 91," alisema.

Alisema UTSS inawafadhili wanafunzi hao ili wafikapo vyuoni waweze kuyafikia malengo yao waliyojiwekea.

Aidha, alisema kwa kipindi cha miaka 12 iliyopita, shirika limeshatoa na kufadhili masomo kwa wanafunzi wenye ualbino 429 ambao wamepata ufadhili kuanzia ngazi ya msingi hadi vyuo vikuu.

Alisema mafunzo wanayotoa kwa vijana hao, yamelenga kuwajengea uelewa wa mazingira ya vyuoni kwa sababu walikotoka walikuwa wanasoma kwenye majengo yaliyozungushiwa uzio lakini sasa wanakwenda kuwa huru.

"Tunawafundisha namna ya utunzaji fedha wawapo vyuoni, lakini pia, watapata fursa ya kutembelea maonyesho ya vyuo vikuu yanayoendelea viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam ili kufanya maombi kwa sababu wengi wao wametoka mikoani, Mwanza, Arusha na Kilimanjaro," alisema.

Shirika hilo pia limewapongeza wanafunzi wenye ulemavu ambao wameweza kufanya vizuri katika mitihani yao ya kitaifa hasa ya kidato cha nne na sita kwa sababu ufaulu wao ni hamasa kwa kundi hilo.

Mnufaika wa kompyuta na mafunzo hayo yanayotowa hivi sasa na shirika hilo, Mwalimu wa Shule ya Msingi Kanyama Wilaya ya Chato mkoani Geita, Marko Sein, alisema atakuwa balozi kwa wenzake kwa kile alichofundishwa.

"Nimefundishwa namna ya kuchangamana na wengine na mimi ni mnufaika wa shirika hili kuanzia mwaka 2013 hadi 2015 wakati nikisoma ualimu ninaishukuru serikali imeniajiri nipo Chato ninafanya kazi, ninamshukuru Peter Ash kwa ufadhili huu," alisema.

Mnufaika mwingine ambaye ni mhitimu wa kidato cha nne, Amina Suleiman mwenye ndoto ya kuwa mwanasheria mwenyeji wa Mwanza, alishukuru shirika hilo kwa udhamini huo wa kompyuta, ambao alisema utamrahisishia kufanya kazi kwa wakati.

# Serikali kuwadhibiti wavunjifu wa amani

**Na Thobias Mwanakatwe**

SERIKALI mkoani Songwe imesema imejipanga kukabiliana na hali yoyote ya uvunjifu wa amani itakayojitokeza wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu, zinazoendelea kote nchini.

Aliwaomba viongozi wa dini mkoani humo kuzitumia nyumba zao za ibada kuhubiri amani na kukemea kwa nguvu zote kauli za upotoshaji zinazotolewa na baadhi ya wanasiasa ili kuendelea kulinda na kudumisha amani.

Mkuu wa Mkoa huo, Brigedia Jenerali Nikodemas Mwangela, alisema hayo juzi katika kikao chake na viongozi wa dini, wazee wa mila, watu maarufu na wafanyabiashara wa Wilaya ya Momba, kilichofanyika Mji wa Tunduma.

Alisema wakati wa mikutano yote ya kampeni kwa vyama vyote, ulinzi wa uhakika utaimarishwa hivyo wananchi wajitokeze ili wapate nafasi ya kuyachuja yale yanayosemwa kwenye majukwaa na wagombea.

Alisema wananchi lazima watambue kuwa jukumu la kulinda amani ya nchi ni la kila Mtanzania, hivyo kila mtu anatakiwa kusimama kwenye nafasi yake.

Alisema jukumu kubwa la serikali ni kuhakikisha kuna amani na utulivu na wananchi wanaendelea na kazi zao za kujiletea maendeleo zinaendelea bila kubughuziwa, kusumbuliwa na kitu chochote.

"Wakati wa janga la corona mlisaidia sana kuliombea taifa, nawaomba muingie tena kwenye maombi kuliombea katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi na sisi kwa upande wetu tutahakikisha lije jua, ije mvua tutahakikisha amani na utulivu vinakuwapo," alisema Mwangela.

Naye msaidizi wa kiongozi wa mila wa kabila la Wanyamwanga, Princewel Mkoma, akiwasilisha ujumbe wa chifu Mkoma katika kikao hicho, alikemea matukio yanayoashiria uvunjifu wa amani katika Mji wa Tunduma.

Ujumbe huo wa chifu Mkoma umekuja ikiwa ni siku chache baada ya kutokea mauaji ya kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Briton Mollel.



Mafundi wakiezeka soko jipya, linalojengwa kwa ajili ya wachuuzi wanaofanya biashara zao, kando ya Barabara ya Morogoro, eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Wahandisi 200 waadhibiwa kukiuka maadili

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Usajili wa Wahandisi (ERB), imesema kuwa imewachukulia hatua wahandisi 264 katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2015 hadi 2020 kutokana na makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa maadili ya taaluma ya kiuhandisi.

Msajili wa Bodi hiyo, Mhandisi Patrick Barozi, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma, kuhusiana na maadhimisho ya Siku ya Wahandisi kwa mwaka huu, ambayo yatafanyika Septemba 3 na 4.

"Bodi imechukua hatua mbalimbali kwa wahandisi 264 ikiwamo kuwaonya na kuwapeleka mahakamani wahandisi ambao walionekana kukiuka kiapo chao cha utii katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, na itaendelea kufuatilia wahandisi ambao hawana maadili lengo ni kuhakikisha wanazingatia maadili ya taaluma yao siku zote," alisema Barozi.

Alifafanua kuwa hatua hiyo itafuatia baada ya wahandisi hao kula kiapo cha utii ambacho kinawakumbusha kuwajibika vyema kwenye taaluma zao na maamuzi yao ya utendaji wao wa kihandisi wa kila siku.

Kuhusu siku hiyo ya wahandisi, alisisitiza kuwa mbali na kuwa na shughuli mbalimbali zitakazofanywa, pia wataalamu watakula kiapo cha utii kama ilivyo kwa miaka mingine ili kufanya wawajibike vyema kwenye taaluma zao.

Alitaja shughuli nyingine zitakazofanyika kuwa ni pamoja na kuwapo kwa kongamano la wahandisi vijana, majadiliano ya kitaaluma, maonyesho mbalimbali ya ubunifu na teknolojia na biashara, kutoa tuzo mbalimbali kwa wahandisi na kampuni, kuwatambua na kuwazawadia wahandisi wahitimu waliofanya vizuri katika mitihani yao ya mwaka wa mwisho wa 2019/2020.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati ya maadhimisho ya Siku ya Wahandisi, Profesa Bakari Mwinyiwiwa, amesema kuwa lengo kuadhimisha siku ya wahandisi ni kuuwezesha umma kutambua michango chanya inayofanywa na wahandisi wa Tanzania katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini.

Alisema kuwa lengo jingine ni kuwatambua wahandisi hao, kampuni na mashirika ya kihandisi yaliyotoa michango mikubwa ya kihandisi katika maendeleo ya taifa na hivyo kuwahamasisha wahandisi wengine kufanya shughuli zao vizuri zaidi.

Maadhimisho ya Siku ya Wahandisi Tanzania kwa mwaka huu ambayo yanafanyika kwa mara ya 17 tangu kuanzishwa kwake yanatarajiwa kushirikisha wahandisi zaidi ya 5,000 kutoka sehemu mbalimbali ikiwamo Zimbabwe, Kenya, Nigeria, Uganda, Rwanda, Misri, Malawi, Botswana na Kenya.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Angalizo la Askofu KKKT uchaguzi lifanyiwe kazi

**WAKATI** vyama vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika Oktoba 28, mwaka huu vikianza kampeni za kuomba kura, wadau kadhaa wametoa angalizo kuhusu lugha za matusi na kashfa.

Wadau mbalimbali wamekuwa wakivitaka vyama vya siasa na wagombea wanaposimama kwenye majukwaa kujikita zaidi kuzungumzia mambo ya maendeleo ambayo watawafanyia wananchi pamoja na mikakati watakayoitumia katika utekelezaji wa ahadi hizo. Kwa ujumla wanavitaka vyama na wagombea kujikita zaidi katika kampeni za kistaarabu badala ya kujielekeza kuwashambulia wagombea wengine na vyama vyao kwa kutumia lugha za matusi, kejeli, vijembe na hata kashfa.

Kampeni zisizo za kistaarabu na zenye kauli za matusi, kejeli, vijembe na kashfa hazina tija kabisa kwa Mtanzania ambaye anakabiliwa na matatizo lukuki, ambayo yanajitaji kupatiwa ufumbuzi. Kwa maneno mengine, Watanzania wanataka kuelezwa jinsi gani watajengewa barabara, madaraja, kupata huduma bora za elimu, afya zikiwamo huduma za bima ya afya.

Ni kweli kwamba wadau kadhaa wamezungumzia masuala haya na kutoa angalizo, lakini kauli za Askofu wa Kanisa la Kiinjili Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Morogoro, Jacob Mameo, ya mwishoni mwa wiki imetoa uzito zaidi na pia kujikita katika kukemea vikali vitendo vya rushwa kwenye uchaguzi.

Askofu Mameo aliwataka wanasiasa wote nchini kufanya siasa za kistaarabu na kuepuka rushwa na matusi katika kipindi hiki cha kampeni za uchaguzi mkuu.

Alisema hayo wakati wa ibada ya ufunguzi wa nyumba ya mchungaji wa kanisa hilo, Usharika wa Lungo, Mvomero mkoani Morogoro, na kuwataka wanasiasa na mashabiki wa siasa kote nchini kuitunza amani ya nchi kwa kuepuka vurugu, matusi na rushwa kwenye majukwaa ya kampeni.

Aliwataka wanasiasa wafanye kampeni zao kistaarabu, waseme sera zao na waache kutukana, maana matusi na vurugu sio sera, na kwamba waseme kile wanachotaka kuwafanyia Watanzania. Kuhusu rushwa, Askofu Mameo alisema wanasiasa waepuke kutoa rushwa kwa kuwa rushwa hupofusha macho, na huondoa uwezo wa kufikiri vema.

Kwamba kiongozi akiwapa rushwa watu ili wamchague, huwafanya watu hao kuchagua pasipo umakini na kwamba rushwa ni adui wa haki, kuchagua au kuchaguliwa kwa misingi ya rushwa huwaondolea watu haki ya kupata kiongozi bora:

Kwa mujibu wa Askofu huyo, wanasiasa ambao huendekeza rushwa, waache kutoa rushwa kwa lengo la kushawishi kuchaguliwa, na kuwa wanaotoa na kupokea rushwa wanapaswa kutubu kwa kuwa rushwa ni dhambi kubwa, ambayo inapaswa kuepukwa kwa kila namna.

Tunakubaliana na angalizo la Askofu Mameo kuhusu rushwa katika uchaguzi kwa sababu vitendo hivyo kuwaondolea wananchi haki yao ya kupata maendeleo kutokana na viongozi waliochaguliwa kwa njia hiyo hukosa dhamana kwa wananchi.


Kiongozi anayechaguliwa kwa rushwa haoni sababu za kuwajibika kuwatumikia wananchi kwa sababu anaamini kuwa kwa kuwapa hongo; ziwe fedha, khanga, pombe na zawadi za aina mbalimbali, anakuwa ameshamalizana nao.

Hiyo inamaanisha kuwa kiongozi huyo hafai na hana msaada kwa wananchi wake kwa kuwa hawezi kuguswa na matatizo pamoja na kero za wananchi kutokana na kuamini kuwa ameshawapa walichotarajia awapatie.

Watanzania wote wanapaswa kutilia maanani angalizo la Askofu Mameo kwa kuwakataa wagombea watakaowapa rushwa kwa lengo la kuwachagua. Kama wakipewa fedha, tunawashauri wazichukue, lakini Oktoba 28 wawakate kwenye sanduku la kura, wachague wagombea ambao watawasaidia kwa dhati ikiwamo kuwatatulia kero na kuwapigania kupata haki za msingi, huduma muhimu za jamii na kuwaletea maendeleo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mwamko huu ni chachu kusonga mbele kisiasa

Na Sabato Kasika

**HISTORIA** inaonyesha kuwa katika harakati za wanawake kuwania urais, mwaka 1995, alijitokeza mwana mama Rose Lugendo ndani ya CCM aliyetia nia ya kutaka nafasi hiyo, lakini kura hazikutosha.

Karata ikamwangukia hayati Rais Benjamini Mkapa, aliyekuwa rais wa awamu tatu, mwaka 2000 hakujitokeza mwanamke kuwania nafasi hiyo ya urais.

Dokta Anna Senkoro, alichomoza kuwania urais kupitia APPT- Maendeleo, ingawa hakufika mbali.

Mwaka 2010 hakuna mwanamama aliyetia nia kwa nafasi hiyo, lakini uchaguzi mkuu wa 2015 Amina Salum Ali ni miongoni mwa watiania CCM waliochomoza na kupata kura zaidi ya 250, lakini karata ikimwendea John Magufuli aliyeteuliwa kuiwakilisha CCM

Anna Mghwira kupitia ACT-Wazalendo ndiye mwanamke aliyepeperusha bendera ya chama chake kwenye uchaguzi huo.

Tangu mwaka 1995, wanawake wanaojitokeza kuwania urais si zaidi ya mmoja, lakini safari hii imekuwa tofauti na uchaguzi mwingine, wanawake wana mwamko zaidi.

Yuko Queen Sendiga wa Alliance for Democratic Change (ADC) na Cecilia Mmanga kutoka Demokrasia Makini, wote wakiwania urais.

Wamepitishwa na vyama vyao na sasa wanaendelea na kampeni kunadi ilani za vyama kwa wapigakura tayari kwa uchaguzi mkuu Oktoba.

Hizi ni sura mpya ambazo huenda Watanzania wengi hawazifahamu kwani si maarufu kama walivyo wanasiasa wengine.

Mmoja wa wana mama hao Queen Sendiga, anataja vipaumbele vyake endapo wananchi watamchagua kuwa ni elimu, afya na sekta ya kilimo.

"Vipaumbele vyangu endapo Watanzania watanipa ridhaa ya kuongoza nchi, nitaanza na elimu kwa kuboresha maslahi ya walimu, ikiwamo mishahara na makazi, nitaongeza vituo vya afya na kusomesha wataalamu wengi zaidi ili kulisaidia taifa," anasema Queen.

Anasema, chama chao kinazingatia usawa wa kijinsia kikiwa kipengele kwenye katiba yake.

Mgombea huyo anasema, baadhi ya vyama vya siasa vimekuwa vikiwakwamisha wanawake kutokana na mfumo dume wa vyama hivyo, lakini chama chao kinajali jinsia zote.

Wakati akiahidi hayo, mwenzake, Cecilia Mwanga, anaahidi kufanya kampeni zake kwa kutumia usafiri wa baiskeli au guta, na kwamba akichaguliwa atasimamia kilimo ili kiwe na tija.

"Nataka kuudhihirishia umma kwamba watakaponichagua, nitahikikisha nawasimamia watu wa hali ya chini, wakulima, hatutawabagua tunataka kunyanyuka nao, na tumejipanga na chama chetu," anasema Mwanga.

Wingi wa wanawake katika uchaguzi wa mwaka huu hauishii kwenye urais tu bali umeanzia katika nafasi ya udiwani na ubunge, ambapo vyama vyao vimewateua kwa wingi tofauti na miaka ya nyuma.

Miaka ya nyuma, wanawake walitegemea nafasi ya viti maalum, lakini safari hii wamejitosa kimasomaso kusimama kuomba kura kwa wananchi katika kata, majimbo na urais.

Vyama vimewateua kwa wingi hali inayoonyesha kutambua mchango wao katika uongozi na kuondoa mazoea ya mfumo dume, ambao umepitwa na wakati, na hautakiwi kukumbatiwa tena.

Katika mchakato wa kusaka wagombea wa nafasi hizo ndani ya vyama, vipo ambavyo vimeteua wanawake zaidi ya 30 kuwania ubunge wa majimbo, uteuzi ambao haujawahi kufanyika katika historia ya siasa ya Tanzania.

### WAGOMBEA URAIS

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imepitisha wagombea 15 wa urais, ambao ni Dk. John Magufuli (CCM), Tundu Lissu (CHADEMA), Bernard Membe (ACT-Wazalendo) na Shibuda Magale (ADA-TADEA).

Wagombea wengine ni Queen Sendga (ADC), Hashim Rungwe (CHAUMMA), Prof. Ibrahim Lipumba (CUF), Cecilia Mwanga (Demokrasia Makini) na Philip Fumbo (DP).

Mbali na hao, wagombea wengine ni Yeremia Maganja (NCCR-Mageuzi), Leopold Mahona (NRA), Muttamwega Mgaywa (SAU), Twalib Ibrahim (UPDP), Mazrui Mohamed (UMD) na Seif Maalim Seif (AAFP).

Katika idadi hiyo, wagombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni wanawake wawili, ingawa wapo wachache, ambao waliteuliwa na vyama vyao kuwania nafasi ya makamu wa rais.

Kujitosa kwa wanawake wawili kuwania urais na kupitishwa na vyama ni hatua inayoonyesha kinamama wameamka.

## RC aagiza kuundwa kamati kumaliza mgogoro wa ardhi

**Na Tiganya Vincent**, TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, amemwagiza Katibu Tawala wa Mkoa kuunda kamati ya kuchunguza mgogoro unaoendelea kwenye mradi wa umwagiliaji katika bwawa la Inala lililoko Manispaa ya Tabora ambao umekuwa ukitishia amani.

Alitoa agizo hilo jana mjini hapa baada ya kutembelea mradi huo kwa lengo la kusikiliza kero ya wakulima wa eneo hilo ili kuzitafutia ufumbuzi.

Dk. Sengati alisema serikali imewekeza zaidi ya Sh. bilioni moja katika mradi huo kwa lengo la kuondoa upungufu wa chakula katika Manispaa ya Tabora badala yake kumekuwapo migogoro ambayo inakwamisha uzalishaji.

Alisema migogoro hiyo imesababishwa na baadhi ya watu wakiwmo viongozi ambao wameweka maslahi binafsi kwa kutaa maeneo ya wananchi.

Dk. Sengati alisema uongozi wa mkoa hauwezi kuona mradi huo wa kimkakati unafia mikononi mwao bila kuchukua hatua.

Alisema kamati hiyo inatakiwa ichunguze kiini cha mgogoro na kutoa mapendekezo ya kuumaliza ndani ya siku saba ili wakulima wa eneo hilo waendelee kufanya kazi zao kwa amani na kuzalisha mazao mengi.

Dk. Sengati alisema kamati hiyo inatakiwa kuwa na wanasheria kutoka ofisi yake, wataalamu kutoka Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na wabobezi wengi ambao watasaidia kutoa mwelekeo kwa kumaliza mgogoro huo.

Pia alisema ni lazima ifanyie uchunguzi wa maeneo ya wananchi yaliyochukuliwa bila kufuata utaratibu ikiwamo yale ambayo Baraza la Madiwani lililoagiza yachukuliwe bila kuwahusisha wahusika.

Aidha, Mkuu wa Mkoa aliwataka viongozi waliopewa jukumu la kuendesha mradi huo kusimamia haki na kuwawezesha wakulima wa eneo hilo kuzalisha kwa wingi.

Alisema serikali haitasita kuwachukulia hatua watumishi na viongozi ambao wamechukua maeneo ya wakulima hao bila kufuata utaratibu unaongoza mradi kwa lengo la kuwanyanyasa wakulima.

# Shamimu, mumewe wana kesi ya kujibu

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Rushwa maarufu kama Mafisadi imesema kwamba mfanyabiashara Abdul Nsembo (45) na mke wake Shamimu Mwasha (41), wana kesi ya kujibu.

Kadhalika, mahakama hiyo imesema wanafamilia hao wataanza kujitetea kesho (Septemba 3).

Uamuzi huo umetolewa jana na mahakama hiyo iliyoketi chini ya Jaji Elinaza Luvanda baada ya kusikiliza mashahidi wanane na vielelezo sita vya Jamhuri.

Hata hivyo, washtakiwa waliieleza mahakama kwamba wanatarajia kuita shahidi mmoja pamoja na wenyewe, utetezi utakuwa na mashahidi watatu.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Veronica Matikila na Wakili wa Serikali Constantine Kakula.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanadaiwa kusafirisha dawa hizo za kulevya, Mei Mosi, mwaka huu, wakiwa eneo la Mbezi Beach, Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam kinyume na sheria ya uhujumu uchumi.




Mkuu wa Wilaya ya Babati Vijijini, Lazaro Twange (kushoto), akipokea msaada wa mabati kutoka kwa Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi (katikati) kwa ajili ya shule tatu za wilaya hiyo, mkoani Manyara. Benki hiyo, ilitoa vifaa vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 51 kwa mikoa ya Geita, Manyara na Tanga. Kulia ni Meneja wa NMB Mkoa wa Manyara, Daniel Rauya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hasunga: Tanzania inakabiliwa uzalishaji mdogo mbegu

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, amesema Tanzania bado inakabiliwa na uzalishaji mdogo wa mbegu bora za mazao na mwaka jana uzalishaji ulifikia tani 71,000 huku mahitaji yakiwa tani 186,000.

Kufuatia hali hiyo, ameiagiza Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), kuongeza uzalishaji zaidi ili kukidhi mahitaji na kuondokana na uagizaji nje ya nchi.

Hasunga alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizindua matrekta saba kwa ajili ya uzalishaji mbegu za mazao ya kilimo unaofanywa na taasisi hiyo.

Alisema matumizi ya mbegu bora nchini bado yapo chini kwa kuwa kwenye maeneo mengi uzalishaji bado upo chini.

"Mwaka jana tumefikia uzalishaji mbegu bora tani 71,000 na mahitaji ni zaidi ya tani 186,000, mbegu zilizopatikana hizo bora bado zaidi ya asilimia 90 zinatokana na uzalishaji wa hapa nchini, mchango mkubwa umefanywa na TARI nawapongeza sana," alisema.

Alisema uagizaji mbegu nje ya nchi ni kuhatarisha usalama wa nchi hivyo ni vyema watafiti wakaongeza jitihada za uzalishaji wa mbegu bora kukidhi mahitaji nchini.

"Tusipokuwa na mbegu tunazoziamini sisi hali ya usalama wa nchi yetu utakuwa hatarini, nyie mmepewa dhamana ya kuhakikisha kunakuwapo na usalama wa mbegu na kugundua zinazofaa kulingana na mazingira ya nchi yetu," alisema.

Alisema matrekta hayo yanalengwa kuongeza uwezo wa TARI kuzalisha mbegu bora kutoka tani 1,000 kwa sasa hadi 10,000 mwaka 2025.

"Vile vile, katika kipindi hicho, TARI itaweza kuzalisha miche kutoka milioni 10.3 ya sasa hadi kufikia miche milioni 40 mwaka 2025, lengo kubwa la mikakati hiyo ni kuhakikisha tunakidhi mahitaji ya mbegu bora kwa wakulima na kupunguza uagizaji wa mbegu toka nje ya nchi," alisema.

Kadhalika, alisema fedha nyingi za kigeni zinatumika kuagiza mafuta ya kula nje ya nchi, kwa sasa serikali inahimiza uzalishaji wa zao la michikichi ili kuongeza uzalishaji nchini.

"Wizara kupitia TARI imezalisha miche milioni mbili kwa mwaka 2019/20 na inategemea kufikia miche milioni 41 mwaka 2025, hatua hizo zinazochukuliwa na serikali zitakidhi mahitaji ya mbegu bora kwa wakulima kwa mwaka na hivyo kupunguza uagizaji wa mafuta ya kula na mbegu toka nje ya nchi," alisema.

Hasunga alisema hatua hiyo itasaidia kupunguza mahitaji makubwa ya mafuta na kuondokana na uagizaji nje ya nchi ili fedha hizo zitumike kufanya miradi mingine.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi hiyo, Dk. Geofrey Mkamilo, alisema matrekta hayo ni moja ya jitihada za kuimarisha uzalishaji mbegu bora ili nchi ijitosheleze kwa mbegu.

"Licha ya kuwapo na taasisi za umma na kampuni binafsi kuzalisha, lakini tumeendelea kuwa na upungufu wa mbegu ili kukidhi mahitaji, wakulima wanahitaji mbegu zaidi, lakini serikali imeamua TARI ichangie katika upatikanaji huo wa mbegu," alisema.

Alisema imebainika kampuni binafsi hazijihusishi na uzalishaji wa mbegu kwenye mazao mengine na wao wanazalisha mbegu za mahindi na maharage kwa kuwa yana thamani kubwa.

"Yapo mazao ambayo sisi kama watafiti tumegundua mbegu nyingi, lakini hazijawafikia wakulima, hivyo tumeona sisi kama TARI tuongeze juhudi kuhakikisha tunazalisha mbegu ili kuwafikia wakulima kama vile michikichi, kuna kampuni ilikuwa inaagiza nje ya nchi na kuwauzia nchini na mche mmoja uliuzwa kwa Sh. 6,000," alisema.

Alisema taasisi hiyo kwa kuliona hilo waliamua kuzalisha mbegu hiyo ili kuwafikia wakulima na kuzalisha mbegu za mihogo, viazi, nazi na korosho.

Pia, alisema katika mwaka wa fedha 2019/20, wizara kupitia TARI iliandaa andiko na kuwasilisha Wizara ya Fedha ili kuboresha miundombinu ya utafiti na uzalishaji mbegu.

Alisema Sh. bilioni 3.06 zimetolewa na kati ya hizo ilitengwa bajeti ya kununua matrekta hayo ili yachangie upatikanaji wa mbegu bora.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001:2015 Certified

*KUMB: PPR/2020 - 09/1*

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 2 SEPTEMBA 2020

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 2 Septemba 2020.** Pamoja na kutambua bei hizo, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

(a) Bei za jumla na rejareja za mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa yaliyopokelewa kupitia **Bandari ya Dar es Salaam** zimeongezeka ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 5 Agosti 2020. Kwa mwezi Septemba 2020, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 20/lita (sawa na asilimia 1.11), Shilingi 8/lita (sawa na asilimia 0.46) na Shilingi 124/lita (sawa na asilimia 7.93). Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli, Dizeli na Mafuta ta Taa zimeongezeka kwa Shilingi 20.19/lita (sawa na asilimia 1.18), Shilingi 8.14/lita (sawa na asilimia 0.49) na Shilingi 123.89/lita (sawa na asilimia 8.58), mtawalia.

(b) Kwa mwezi Septemba 2020, bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli **kwa Mikoa ya Kaskazini** (Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara) zimepungua ukilinganisha na bei zilizotolewa tarehe 5 Agosti 2020. Kwa mwezi Septemba, bei za rejareja za Petroli na Dizeli zimepungua kwa shilingi 19/lita (sawa na asilimia 1.04) na shilingi 5/lita (sawa na asilimia 0.25), mtawalia. Vilevile, ukilinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli zimepungua kwa shilingi 19.35/lita (sawa na asilimia 1.11) na shilingi 4.51/lita (sawa na asilimia 0.27), mtawalia. Hata hivyo, bei za mafuta ya taa hazina mabadiliko na zitaendelea kuwa zile zilizotangazwa katika toleo lililopita la tarehe 5 Agosti 2020. Hii ni kwa sababu, kwa mwezi Agosti 2020 hakuna shehena ya mafuta iliyopokelewa nchini kupitia bandari ya Tanga.

(c) Kwa mwezi Septemba 2020, bei za rejareja na jumla kwa bidhaa za mafuta ya Petroli na Dizeli kwa **Mikoa ya Kusini (Mtwara, Lindi, and Ruvuma)** zimeongezeka ukilinganisha na bei zilizotolewa tarehe 5 Agosti 2020. Kwa mwezi Septemba, bei za rejareja za Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa shilingi 11/lita (sawa na asilimia 0.60) na Shilingi 16/lita (sawa na asilimia 0.91), mtawalia. Vilevile, ukilinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa shilingi 11.19/lita (sawa na asilimia 0.64) na shilingi 16.36/lita (sawa na asilimia 0.98), mtawalia.

(d) Mabadiliko ya bei za mafuta katika soko la ndani yanatokana na mabadiliko ya bei za mafuta katika soko la dunia, gharama za usafirishaji **(BPS Premium)** na gharama za ucheleweshaji wa ushushaji wa mafuta **(Demurrage cost).**

(e) EWURA inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.

(f) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.

(g) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (price cap)** kama ilivyokokotolewa na kanuni (formula) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 74 la tarehe 7 Februari 2020.**

(h) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**

(i) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP **(Electronic Fiscal Pump Printers)** na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya mafuta ya petroli.

# TANGAZO

## JEDWALI A: BEI ZA REJAREJA

| Mji | Bei Kikomo | | |
|---|---|---|---|
| | Petroli (Shs/Lita) | Dizeli (Shs/Lita) | Mafuta Ya Taa (Shs/Lita) |
| **Dar es Salaam** | **1,852** | **1,793** | **1,692** |
| **Arusha** | **1,905** | **1,830** | **2,044** |
| Arumeru (Usa River) | 1,905 | 1,830 | 2,044 |
| Karatu | 1,924 | 1,848 | 2,062 |
| Longido | 1,916 | 1,841 | 2,055 |
| Monduli | 1,911 | 1,835 | 2,049 |
| Monduli-Makuyuni | 1,915 | 1,840 | 2,054 |
| Ngorongoro (Loliondo) | 1,990 | 1,915 | 2,128 |
| **Pwani (Kibaha)** | **1,857** | **1,797** | **1,697** |
| Bagamoyo | 1,863 | 1,804 | 1,703 |
| Bagamoyo (Miono) | 1,894 | 1,835 | 1,734 |
| Chalinze Junction | 1,866 | 1,807 | 1,706 |
| Chalinze (Msata) | 1,871 | 1,811 | 1,710 |
| Kibiti | 1,873 | 1,813 | 1,713 |
| Kisarawe | 1,859 | 1,800 | 1,699 |
| Mkuranga | 1,862 | 1,803 | 1,702 |
| Rufiji | 1,880 | 1,820 | 1,720 |
| **Dodoma** | **1,911** | **1,852** | **1,751** |
| Bahi | 1,918 | 1,859 | 1,758 |
| Chamwino | 1,906 | 1,847 | 1,746 |
| Chemba | 1,937 | 1,878 | 1,777 |
| Kondoa | 1,944 | 1,884 | 1,784 |
| Kongwa | 1,908 | 1,849 | 1,748 |
| Mpwapwa | 1,912 | 1,853 | 1,752 |
| Mtera (Makatopora) | 1,930 | 1,871 | 1,770 |
| Mvumi | 1,917 | 1,858 | 1,757 |
| **Geita** | **2,018** | **1,958** | **1,858** |
| Bukombe | 2,007 | 1,947 | 1,847 |
| Chato | 2,039 | 1,979 | 1,879 |
| Mbogwe | 2,056 | 1,996 | 1,896 |
| Nyang'hwale | 2,033 | 1,973 | 1,873 |
| **Iringa** | **1,916** | **1,857** | **1,756** |
| Ismani | 1,922 | 1,862 | 1,761 |
| Kilolo | 1,921 | 1,861 | 1,761 |
| Mufindi (Mafinga) | 1,926 | 1,867 | 1,766 |
| Mufindi (Igowole) | 1,935 | 1,876 | 1,775 |
| **Kagera (Bukoba)** | **2,068** | **2,008** | **1,908** |
| Biharamulo | 2,042 | 1,983 | 1,882 |
| Karagwe (Kayanga) | 2,084 | 2,025 | 1,924 |
| Kyerwa (Ruberwa) | 2,090 | 2,031 | 1,930 |
| Muleba | 2,068 | 2,008 | 1,908 |
| Ngara | 2,056 | 1,996 | 1,895 |
| Misenyi | 2,076 | 2,017 | 1,916 |
| **Katavi (Mpanda)** | 2,060 | 2,001 | 1,900 |
| Mlele (Inyonga) | 2,079 | 2,020 | 1,919 |
| Mpimbwe (Majimoto) | 2,053 | 1,994 | 1,893 |
| Tanganyika (Ikola) | 2,078 | 2,019 | 1,918 |
| **Kigoma** | **2,084** | **2,024** | **1,924** |
| Uvinza (Lugufu) | 2,096 | 2,037 | 1,936 |
| Buhigwe | 2,073 | 2,013 | 1,913 |
| Kakonko | 2,041 | 1,981 | 1,881 |
| Kasulu | 2,070 | 2,010 | 1,910 |
| Kibondo | 2,048 | 1,989 | 1,888 |
| **Kilimanjaro (Moshi)** | **1,895** | **1,820** | **2,033** |
| Hai (Bomang'ombe) | 1,898 | 1,823 | 2,037 |
| Mwanga | 1,888 | 1,813 | 2,027 |
| Rombo (Mkuu) | 1,912 | 1,836 | 2,050 |
| Same | 1,881 | 1,806 | 2,020 |
| Siha (Sanya Juu) | 1,901 | 1,826 | 2,040 |
| **Lindi** | **1,900** | **1,829** | **1,751** |
| Lindi-Mtama | 1,905 | 1,834 | 1,769 |
| Kilwa Masoko | 1,924 | 1,853 | 1,726 |
| Liwale | 1,936 | 1,865 | 1,772 |
| Nachingwea | 1,920 | 1,849 | 1,780 |
| Ruangwa | 1,927 | 1,856 | 1,782 |
| **Manyara (Babati)** | **1,939** | **1,864** | **2,078** |
| Hanang (Katesh) | 1,950 | 1,875 | 2,088 |
| Kiteto (Kibaya) | 1,955 | 1,879 | 2,093 |
| Mbulu | 1,952 | 1,877 | 2,091 |
| Simanjiro (Orkasumet) | 1,971 | 1,896 | 2,110 |
| **Mara (Musoma)** | **2,031** | **1,971** | **1,871** |
| Musoma Vijijini (Busekela) | 2,072 | 2,012 | 1,911 |
| Rorya (Ingirijuu) | 2,040 | 1,980 | 1,880 |
| Rorya (Shirati) | 2,074 | 2,015 | 1,914 |
| Bunda | 2,022 | 1,963 | 1,862 |
| Bunda (Kisorya) | 2,032 | 1,972 | 1,871 |
| Butiama | 2,028 | 1,968 | 1,868 |
| Serengeti (Mugumu) | 2,076 | 2,017 | 1,916 |
| Tarime | 2,042 | 1,983 | 1,882 |
| Tarime (Kewanja/Nyamongo) | 2,046 | 1,987 | 1,886 |
| **Mbeya** | **1,959** | **1,900** | **1,799** |
| Chunya | 1,969 | 1,909 | 1,809 |
| Chunya (Makongolosi) | 1,983 | 1,924 | 1,823 |
| Kyela | 1,975 | 1,916 | 1,815 |
| Mbarali (Rujewa) | 1,943 | 1,884 | 1,783 |
| Rungwe (Tukuyu) | 1,968 | 1,909 | 1,808 |
| **Morogoro** | **1,877** | **1,818** | **1,717** |
| Mikumi | 1,893 | 1,833 | 1,733 |
| Kilombero (Ifakara) | 1,915 | 1,856 | 1,755 |
| Kilombero (Mlimba) | 1,937 | 1,878 | 1,777 |
| Kilombero (Mngeta) | 1,927 | 1,867 | 1,767 |
| Ulanga (Mahenge) | 1,926 | 1,866 | 1,766 |
| Malinyi | 1,936 | 1,877 | 1,776 |
| Kilosa | 1,896 | 1,836 | 1,736 |
| Gairo | 1,896 | 1,836 | 1,736 |
| Mvomero (Wami Sokoine) | 1,888 | 1,828 | 1,728 |
| Mvomero (Sanga Sanga) | 1,877 | 1,818 | 1,717 |
| Turiani | 1,902 | 1,843 | 1,742 |
| **Mtwara** | **1,887** | **1,816** | **1,765** |
| Nanyumbu (Mangaka) | 1,923 | 1,852 | 1,813 |
| Masasi | 1,903 | 1,832 | 1,790 |
| Newala | 1,908 | 1,837 | 1,797 |
| Tandahimba | 1,901 | 1,830 | 1,790 |
| Nanyamba | 1,901 | 1,830 | 1,790 |
| **Mwanza** | **2,002** | **1,943** | **1,842** |
| Kwimba | 2,020 | 1,961 | 1,860 |
| Magu | 2,010 | 1,951 | 1,850 |
| Misungwi | 1,997 | 1,937 | 1,837 |
| Sengerema | 2,035 | 1,975 | 1,875 |
| Ukerewe | 2,062 | 2,003 | 1,902 |
| **Njombe** | **1,945** | **1,885** | **1,785** |
| Njombe (Kidegembye) | 1,965 | 1,906 | 1,805 |
| Ludewa | 1,983 | 1,923 | 1,823 |
| Makambako | 1,937 | 1,878 | 1,777 |
| Makete | 1,976 | 1,916 | 1,815 |
| Wanging'ombe (Igwachanya) | 1,942 | 1,883 | 1,782 |
| **Rukwa (Sumbawanga)** | **2,025** | **1,966** | **1,865** |
| Sumbawanga Rural (Mtowisa) | 2,025 | 1,966 | 1,865 |
| Kalambo (Matai) | 2,032 | 1,973 | 1,872 |
| Nkasi (Namanyele) | 2,039 | 1,979 | 1,879 |
| **Ruvuma (Songea)** | **1,972** | **1,901** | **1,816** |
| Mbinga | 1,985 | 1,914 | 1,849 |
| Namtumbo | 1,963 | 1,892 | 1,845 |
| Nyasa (Mbamba Bay) | 2,010 | 1,939 | 1,859 |
| Tunduru | 1,938 | 1,867 | 1,875 |
| **Shinyanga** | **1,981** | **1,922** | **1,821** |
| Kahama | 1,995 | 1,935 | 1,835 |
| Kishapu | 2,010 | 1,950 | 1,850 |
| Ushetu (Nyamilangano) | 2,012 | 1,953 | 1,852 |
| **Simiyu (Bariadi)** | **2,023** | **1,963** | **1,863** |
| Busega (Nyashimo) | 2,016 | 1,956 | 1,856 |
| Itilima (Lagangabilili) | 2,026 | 1,966 | 1,866 |
| Maswa | 2,014 | 1,955 | 1,854 |
| Meatu (Mwanhuzi) | 2,021 | 1,962 | 1,861 |
| **Singida** | **1,943** | **1,884** | **1,783** |
| Iramba | 1,955 | 1,896 | 1,795 |
| Manyoni | 1,927 | 1,868 | 1,767 |
| Ikungi | 1,938 | 1,879 | 1,778 |
| Mkalama (Nduguti) | 1,967 | 1,908 | 1,807 |
| **Songwe (Vwawa)** | **1,969** | **1,909** | **1,809** |
| Songwe (Mkwajuni) | 1,975 | 1,916 | 1,815 |
| Ileje | 1,972 | 1,913 | 1,812 |
| Momba (Chitete) | 1,978 | 1,918 | 1,818 |
| Tunduma | 1,973 | 1,913 | 1,813 |
| **Tabora** | **2,006** | **1,947** | **1,846** |
| Igunga | 1,960 | 1,901 | 1,800 |
| Kaliua | 2,025 | 1,966 | 1,865 |
| Ulyankulu | 2,020 | 1,960 | 1,860 |
| Nzega | 1,971 | 1,912 | 1,811 |
| Sikonge | 2,018 | 1,959 | 1,858 |
| Urambo | 2,020 | 1,960 | 1,860 |
| Uyui | 2,007 | 1,948 | 1,847 |
| **Tanga** | **1,849** | **1,773** | **1,987** |
| Handeni | 1,869 | 1,794 | 2,008 |
| Kilindi | 1,884 | 1,809 | 2,023 |
| Korogwe | 1,861 | 1,786 | 1,999 |
| Lushoto | 1,870 | 1,795 | 2,009 |
| Mkinga (Maramba) | 1,856 | 1,780 | 1,994 |
| Muheza | 1,854 | 1,778 | 1,992 |
| Pangani | 1,855 | 1,780 | 1,994 |

## JEDWALI B: BEI ZA JUMLA

| | Petroli (Shs/Lita) | Dizeli (Shs/Lita) | Mafuta ya Taa (Shs/Lita) |
|---|---|---|---|
| DAR ES SALAAM | 1,727.29 | 1,667.76 | 1,567.97 |
| TANGA | 1,723.84 | 1,648.43 | 1,862.19 |
| MTWARA | 1,761.75 | 1,690.60 | - |

**Mha. Godfrey H. Chibulunje**
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**
**EWURA"**

215882402

# Wanafunzi waondokana na adha ya vyoo

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

ADHA iliyowakumba baadhi ya wanafunzi wa shule za msingi Nyaishozi, Kyanyamisa na Kahanga zilizoko Tarafa ya Nyaishozi wilayani Karagwe mkoani Kagera, ya kutumia vyoo visivyo na ubora, imepungua baada ya Shirika la World Vision Tanzania kujenga matundu 24 ya vyoo katika shule hizo.

Baadhi ya vyoo vilikosa ubora ikiwamo kutokuwa na milango.

Wakizungumza na Nipashe wakati wa kukabidhiwa matundu hayo ya vyoo, baadhi ya wanafunzi akiwamo Afta Aron anayesoma darasa la sita katika Shule ya Msingi Kyanyamisa, alisema mbali na uchache wa vyoo vilivyopo, pia wamekuwa wakilazimika kutumia sketi zao kujifunika wakati wa kujisaidia kutokana na vyoo kutokuwa na milango.

Naye Sabato Byamungu wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Kahanga, alisema kutokana na uchache wa matundu ya vyoo, wanafunzi wa kiume wamekuwa wakibanana katika choo kimoja hasa wakati wa haja ndogo, na kuwa wasichana wamekuwa wakilazimika kukimbia vichakani kujisaidia.

**Shule ina wanafunzi 1,032 wakiwamo wa kiume 503 na wa kike 529 na wote walitegemea matundu 12 ya vyoo, tunashukuru kwa kuongezewa matundu manane ya vyoo.**

Pia Rostabela Jovenary, wa darasa la saba Shule ya Msingi Kyanyamisa alisema wakati mwingine wanafunzi wenzake walikuwa wakimchungulia akijisaidia, hali iliyomfanya kuhisi aibu, huku akidai vyoo hivyo pia vilimsababishia magonjwa yanayoambukizwa kwa njia ya mkojo kama UTI.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kyanyamisa, Guidence Mashanda, alisema walikuwa na hali mbaya ya vyoo na kuwa vyoo vya wasichana ilikuwa ni wastani wa wanafunzi 80 kwa tundu moja.

Alisema vyoo vilipokuwa vikikaribia kujaa hasa katika msimu wa mvua walitoa wadudu na kusambaa hali iliyohatarisha afya za wanafunzi na wakati mwingine kuwasababishia magonjwa ya kuhara.

Naye mwalimu mkuu msaidizi wa Shule ya Msingi Kahanga, Simon Richard, alisema katika shule yake ilikuwa ni wastani wa wanafunzi 86 kwa tundu moja la choo, hali iliyosababisha msongamano katika vyoo.

"Shule ina wanafunzi 1,032 wakiwamo wa kiume 503 na wa kike 529 na wote walitegemea matundu 12 ya vyoo, tunashukuru kwa kuongezewa matundu manane ya vyoo," alisema.

Mwakilishi wa World Vision Kanda ya Kagera, Joseph Potino, alisema wamekabidhi matundu 24 ya vyoo katika shule hizo na chumba kimoja cha darasa katika Shule ya Msingi Ruhita, vyote vikiwa na thamani ya shilingi milioni 110.5.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe, Angela Anselimi, alisema serikali inaendelea kufanya kila jitihada ili kuhakikisha wanapunguza tatizo la uhaba wa vyoo shuleni, kwa kushirikisha halmashauri za vijiji na wananchi.



Msanii Giveni Mwasyoge, akitengeneza sanamu ya twiga kwa kutumia saruji na mchanga katika eneo la Goba, jijini Dar es Salaam jana. Sanamu moja ya twiga huiuza kwa Sh. 650,000. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wataka mazingira bora ya kujifungulia

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WARAGHIBISHI wa kamati ya taarifa na maarifa ilioundwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP - Mtandao ), wameiomba Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro kuboresha huduma za vyoo kwa wajawazito upande wa kujifungua kwenye zahanati ili kuheshimu utu wa mwanamke anapotoka kujifungua.

Waraghibishi wa kamati ya taarifa na maarifa iliyoundwa na TGNP- Mtandao wilayani Morogoro, walitoa ombi hilo wakati wakichambua bajeti kwa mrengo wa kijinsia 2020/21 kwenye sekta afya, kilimo na elimu na kusema ipo haja kuangalia changamoto ya wazazi iliyopo kwenye zahanati zote wilayani humo ambayo ni ukosefu wa choo cha ndani na kulazimika kutumia choo cha nje baada ya kujifungua kwa ajili ya kujisaidia.

Waliishukuru serikali katika halmashauri yao kuweka utaratibu wa kujifungua kwenye zahanati unaowaondolea adha ya kupoteza watoto na kutishia uhai wao, lakini walisema si jambo jema kwa mzazi aliyetoka kujifungua kutembea hadi choo cha nje kwa ajili ya mahitaji yake, na kwamba kitendo hicho kinashusha utu wa mwanamke.

Sinahamu Swala, mjumbe kutoka kituo cha taarifa na maarifa Kata ya Mngazi, aliomba halmashauri hiyo kuona haja ya kuweka zamu za waganga kwenye zahanati ili waweze kupata tiba nyakati za usiku kutokana na kukabiliwa na changamoto ya ukosefu wa waganga nyakati za usiku kwenye zahanati na kusababisha usumbufu kwao.

Mwakilishi wa Mganga Mkuu wa wilaya hiyo, Frank Njau, alikiri kuwapo kwa tatizo la ukosefu wa vyoo vya ndani kwenye kila zahanati wilayani humo, na kusema watalifanyia kazi.

Alisema suala la ukosefu wa waganga nyakati za usiku kwenye zahanati linaweza kupungua endapo watapata ongezeko la watumishi.

Aidha, alisema wanaendelea kuboresha wodi za wazazi kwenye vituo vya afya ili kupatikana kwa huduma nzuri.

# NMB yatoa vifaa vya elimu, afya mikoa 3

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imetoa msaada wa vifaa mbalimbali kwenye sekta ya elimu na afya kwa Wilaya ya Bukombe Mkoa wa Geita, Babati mkoani Manyara na Lushoto - Tanga vyenye thamani ya Sh. milioni 51.

Vifaa hivyo vilipokelewa na wakuu wa wilaya hizo mwishoni mwa wiki, ambapo katika Wilaya ya Bukombe NMB ilitoa mabati 200, vitanda 5 na vifaa vya usafi vyenye thamani ya Sh. milioni 10.

Akikabidhi vifaa hivyo kwa mkuu wa wilaya ya hiyo, Said Nkumba, Meneja wa Benki hiyo Kanda ya Magharibi, Sospeter Magesse, alisema benki imetoa vifaa hivyo ili kuhakikisha wanarejesha kwa jamii faida inayopatikana.

Magesse alisema vifaa vilivyotolewa vikiwamo vitanda vitano na vifaa vya usafi ni kwa ajili ya Kituo cha Afya Ushirombo ni pamoja na mabati 200 kwa ajili ya Shule ya Msingi Azimio iliyoko Kata ya Bulangwa.

Akipokea vifaa hivyo, DC Nkumba aliipongeza NMB kwa kuona umuhimu wa kutatua changamoto zinazoikabili jamii ikiwamo kwenye sekta ya elimu na afya.

Katika Wilaya ya Babati Vijijini mkoani Manyara benki hiyo ilitoa mashuka, vitanda, vifaa vya usafi, pamoja na mabati vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 21.

Akikabidhi vifaa hivyo kwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Lazaro Twange, Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi, alisema benki hiyo imetoa vifaa vya afya kwa ajili ya Zahanati ya Merr.

Aidha, alisema imetoa mabati kwa ajili ya shule tatu za wilaya humo, ili kukamilisha ujenzi wa madarasa kwenye shule hizo na kupunguza changamoto ya uchache wa vyumba vya madarasa.

DC Twange aliishukuru benki hiyo kwa msaada huo na kuwa utapunguza kwa kiasi kikubwa changamoto ambazo zilikuwa zikikabili taasisi hizo.

Katika Wilaya ya Lushoto mkoani Tanga benki hiyo imetoa madawati, viti, vitanda pamoja na mabati vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 20.

Meneja wa Kanda ya Kaskazini, Aikansia Muro, akikabidhi vifaa hivyo kwa Mkuu wa Wilaya hiyo, January Lugangika, alisema benki hiyo imetoa mabati 600 kwa ajili ya ujenzi wa shule za msingi Kireti, Kivumo, Nywelo.

Aidha, Muro alisema kuwa benki hiyo imetoa vitanda vya wagonjwa vitatu, vya kujifungulia wazazi na mashuka 20 kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Kwanguruwe.

## Amani ni wajibu kuelekea uchaguzi mkuu wa 2020



Ukurasa 12



Ukurasa 14

## Kamala Harris

siasa
JUMATANO SEPTEMBA 2, 2020
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe

# CCM ilipotangaza 'pepo' ya Tanzania

- Kutengeneza ajira 8,000,000
- Wakulima kumwagiwa pembejeo kilimo



Mgombea urais wa CCM, Rais Magufuli akizindua kampeni jijini Dodoma wiki iliyopita. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Gwamaka Alipipi**

CCM imeingia kazini rasmi, ni baada ya kuzindua kampeni za urais, ubunge na udiwani kwa kishindo mjini Dodoma, huku mgombea wake, Rais John Magufuli akimwaga ahadi lukuki kwa Watanzania.

Inazindua kampeni zake Jumamosi Agosti 29, katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma , kwa kuainisha mengi, makubwa na mazuri, mgombea atakayoifanyia nchi endapo atachaguliwa tena kuongoza, mathalani...

**KUONGEZA NDEGE**

Mojawapo ya ahadi anazozitoa wakati wa uzinduzi wa kampeni ni kuendelea kuimarisha usafiri wa anga, kwa kununua ndege mpya tano ikiwamo ya mizigo.

Akijinasibu mbele ya maelfu ya wananchi waliojitokeza siku hiyo, Rais Magufuli anasema kati ya ndege nne za abiria atakazonunua, mbili zitakuwa za masafa marefu na nyingine zitafanya safari za karibu.

**AJIRA ZA KUTOSHA**

Kwenye hotuba yake Rais Magufuli anawahakikishia Watanzania kuwa serikali itatengeneza ajira takribani 8,000,000 kwenye sekta za kipaumbele ambazo zitasimamiwa ili uchumi wa taifa na Watanzania uzidi kusonga mbele.

UWANJA WA MICHEZO

Mgombea wa CCM anawaahidi wakazi wa jiji la Dodoma kwamba atakapochaguliwa tena kuliongoza taifa, kazi yake ya kwanza itakuwa ni kujenga uwanja mwingine mpya ili wananchi watakapoingia wapate nafasi na kuondoa tatizo la watazamaji wengine kubaki nje.

"Mtakaponichagua lazima nijenge uwanja mkubwa wa michezo na hiyo ndiyo kazi yangu ya kwanza ili wananchi wakiingia wapate nafasi na wote waenee badala ya wengine kukaa nje. Kweli leo tumefunga kazi hii inadhihirisha wazi kuwa hapa ni makao makuu ya nchi,"anasema Rais Magufuli.

**RELI YA KISASA**

Mbali na kutoa ahadi zinazowapa watu tumaini jema , Rais Magufuli anaahidi kujenga reli ya kisasa (SGR) inayoanzia Mwanza hadi Isaka na kutoka Isaka inaifikisha Makutupora jijini Dodoma.

Anasema kuanza kwa ujenzi huo ni mwendelezo wa kujenge reli ya kisasa uliokwishaanza kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro yenye urefu wa kilometa 300 na kutoka Morogoro hadi Makutupora kilometa 422 kwa gharama ya Sh. trilioni saba.

**MELI ZA SHEHENA**

Kadhalika, Rais Magufuli akiwahutubia wananchi waliojitokeza katika kampeni hizo, anasema akiingia madarakani katika awamu nyingine atahakikisha taifa linanunua meli za shehena zitakazofanyakazi katika bahari ya Hindi na Ziwa Tanganyika na meli ya kubeba makasha (makontena) Ziwa Victoria na upanuzi wa bandari baharini na kwenye maziwa.

"Lengo tutekeleze mambo makubwa tuliyoweka kwa kasi zaidi, hivyo nawaomba sana siku ya uchaguzi ni siku muhimu ya kuitengeneza nchi. Mimi na wenzangu tunaamini tutanadi yale tuliyofanya ili nchi isonge mbele.Tupeni tena miaka mitano tukawafanyie makubwa zaidi Watanzania. Mambo mazuri na makubwa yanakuja, tuendelee kuwa wamoja," anasisitiza Rais Magufuli na kuongeza:

"Watakuja wengi, wasikilizeni, lakini siku ya kupiga kura kuweni makini, uchaguzi huu ni muhimu sana, Watanzania naomba kura zenu kwa urais, wabunge na madiwani wa CCM ili tukayatekeleze tunayoahidi kwa kasi zaidi."

**KUPAMBANA NA RUSHWA**

Rais Magufuli anasema serikali yake kupitia CCM itaendelea kudhibiti na kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa, uhujumu uchumi na ufisadi kwa miaka mitano ijayo.

Aidha, mgombea huyo wa urais anaeleza kuwa akiingia madarakani tena serikali atakayoiunda itaendelea kudhibiti na kuimarisha mapambano dhidi ya uzalishaji, uingizaji, usambazaji, uuzaji na matumizi ya dawa za kulevya, utakatishaji wa fedha haramu na biashara ya kusafirisha binadamu.

**MUUNGANO KWANZA**

Rais Magufuli anawahakikishi Watanzania kuwa miaka mitano ijayo atahakikisha anaendelea kulinda, kuimarisha na kudumisha uhuru, mapinduzi matukufu ya Zanzibar na Muungano wa Tanzania.

"Kuendelea kulinda na kuimarisha demokrasia ya vyama vingi, haki za binadamu, nchi isiyofungamana na dini yoyote na kupambana na unyanyasaji na udhalilishaji wa aina zote," anaahidi Rais Magufuli.

Mbali na jukumu la kuimarisha Muungano, Rais Magufuli pia anaahidi kuendelea kuhakikisha Tanzania inakuwa nchi isiyofungamana na upande wowote, ili kutetea na kulinda maslahi ya taifa kwa kuzingatia misingi inayoamini.

"Kuimarisha utumishi wa umma, unaozingatia weledi, nidhamu, uadilifu, bidii na maarifa katika kazi, kuimarisha mifumo ya kisera, kitaasisi na kisheria ikiwamo kutungwa kwa sheria inayotaka serikali za mitaa kutenga asilimia 10 ya mapato yake kwa ajili ya uwezeshaji wa wanawake asilimia nne, vijana asilimia nne, watu wenye ulemavu asilimia mbili," alisema Rais Magufuli.

**UCHUMI WA VIWANDA**

Kadhalika, anaeleza kuwa serikali yake itaendelea kujikita zaidi kuimarisha uchumi wa viwanda na kwamba mwaka 2015 kulikuwa na viwanda 52,633 lakini hadi kufikia mwaka jana vimeongezeka na kufikia 61,110, ikiwa ni ongezeko la asilimia 16.1.Halikadhalika anasisitiza kutokomeza umasikini, kuondoa tatizo la ajira.

**UHAKIKA PEMBEJEO**

Kwenye sekta ya kilimo, Rais Magufuli anaahidi upatikanaji wa pembejeo, zana za kilimo pamoja na kuiboresha Benki ya Kilimo, kuipanua sekta ya umwagiliaji, kuimarisha huduma za ugani pamoja na vyama vya ushirika.

Anazungumzia uhamasishaji na ufugaji wa kisasa, upatikanaji wa dawa na chanjo kwa ajili ya mifugo, ujenzi wa bandari ya uvuvi pamoja na kununua meli za uvuvi.

Awali, Rais Magufuli anaeleza mafanikio mbalimbali yaliyopatikana katika serikali yake kwenye awamu ya kwanza ya uongozi wake. Baadhi ya mafanikio hayo ni kutoa elimu bure kuanzia shule ya msingi hadi kidato cha nne.



Maalim Seif Sharif Hamad, **PICHA MTANDAO.**

# AMANI NI WAJIBU KUELEKEA UCHAGUZI MKUU

**Na Dk. Enock Mlyuka**

KAMPENI kwa ajili ya uchaguzi mkuu zimeshaanza rasmi huku vyama vilivyoweka wagombea kwa nafasi ya urais, ubunge, udiwani na uwakilishi vikinadi sera zao ili kushawishi wananchi wavichague katika uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Pamoja na kuanza kwa kampeni hizo, baadhi ya wagombea na viongozi wa vyama vya siasa, wameanza kutoa kauli na matamko ambayo yanaashiria chuki na uvunjifu wa amani.

Kutokana na hali hiyo, ni vyema Watanzania wakaendelea kukumbushwa umuhimu wa kudumisha amani, umoja na mshikamano uliodumu kwa miaka mingi tangu kuasisiwa kwa taifa. Pia wanapaswa kujizatiti katika ujenzi wa jamii inayosimikwa katika msingi wa haki, amani na utulivu kwa ajili ya ustawi na maendeleo ya taifa.

Haki na amani ni mapacha wasiotengana. Haki inahusika zaidi katika kuleta amani na uhusiano mzuri kati ya wanadamu, kati ya mwanadamu na uumbaji na utamaduni wa aina mbalimbali. Hivyo, tunda la haki ni amani na mahali penye amani hutazamiwa kuwa na utulivu.

Kama inavyofahamika, haki ni suala mtambuka lenye kubeba mambo mengi. Kwa kutaja mambo machache; watu wana haki ya kuishi na kuwa na maisha mazuri yenye heshima na nidhamu; haki ya kulindwa katika maisha yao; haki ya kushiriki katika shughuli za maendeleo; haki ya kumwabudu Mungu kadiri ya imani na dhamira zao; haki ya kuchagua hali ya maisha wanayoyapenda zaidi;haki ya kuchagua viongozi wanaowataka; haki ya kuwa huru katika kutafuta ukweli.

Ni jambo la msingi kufahamu kuwa siku zote haki huenda pamoja na upendo. Haki pasipo upendo ni unafiki na dalili ya kukaa ndani ya kifo. Amani ni moja ya matunda ya haki na zawadi kutoka kwa Mungu inayomwajibisha binadamu. Amani ni msingi wa wema, heshima na maendeleo endelevu na fungani ya binadamu.

Kwa mantiki hiyo, amani ni tunda linalopaswa kutunzwa kwa njia ya malezi ya dhamira nyofu; ukweli na uhuru, lakini uhuru wenye mipaka; usalama wa raia na mali zao; kwa kulinda na kuheshimu utu wa binadamu, ustawi na maendeleo.

Kwa hiyo, katika kuelekea uchaguzi mkuu, wananchi na viongozi hawana budi kujizatiti katika ujenzi wa jamii inayosimikwa katika msingi wa haki, amani na utulivu kwa ajili ya ustawi na maendeleo ya taifa.

Vyombo vya ulinzi na usalama vinapaswa kutimiza wajibu wao kwa weledi na kuepuka vitendo vya upendeleo na uonevu. Kwa upande mwingine, wanasiasa na wananchi wanao wajibu wa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo mbalimbali iliyotolewa kuhusu uchaguzi ili kutolazimisha vyombo vya ulinzi na usalama kutumia nguvu pale watakapojiridhisha kuwa kuna kauli na vitendo vya upotoshaji wa wananchi na vyenye dalili ya kuondosha amani na utulivu. Kimsingi, wananchi wanatazamia kuona siasa safi kwani huo ni msingi wa maendeleo. Maendeleo ya nchi yanategemea uwapo wa haki, amani na utulivu katika jamii.

> Kwa mantiki hiyo, amani ni tunda linalopaswa kutunzwa kwa njia ya malezi ya dhamira nyofu; ukweli na uhuru, lakini uhuru wenye mipaka; usalama wa raia na mali zao; kwa kulinda na kuheshimu utu wa binadamu, ustawi na maendeleo.

Wakati wa kampeni, wagombea hawana budi kujikita katika hoja zenye mashiko na huduma kwa wananchi. Siasa ni sehemu ya vinasaba vya maisha ya binadamu na kwamba siasa safi hutekelezwa kwa kufuata na kuzingatia Katiba, sheria, kanuni za maadili, mambo ambayo ni msingi katika kukuza demokrasia na kudumisha misingi ya amani, haki, ustawi na maendeleo ya nchi.

Pia ni muhimu ikafahamika kuwa siasa safi ni kielelezo cha hali ya juu cha upendo katika jamii. Matunda ya ukomavu yanayohitajika katika uongozi bora, utawala wa sheria, uvumilivu, uaminifu na bidii.

Kamwe tofauti za kiitikadi kisiwe chanzo cha vurugu na mpasuko katika jamii kwani hali hii inaweza kuliangamiza taifa. Watu wanapaswa kuheshimiana na kuthaminiana hata katika tofauti walizo nazo ili kulinda utu, heshima na haki za binadamu.

Tume ya Uchaguzi imebeba dhamana kubwa ya uchaguzi mkuu, hivyo ina wajibu wa kuhakikisha uchaguzi unakuwa huru, wa wazi, haki na amani, huku tume yenyewe ikiwa kielelezo katika kusimamia sheria, taratibu na Kanuni za maadili ya uchaguzi. Kadhalika, mahakama zinapaswa kutenda haki wakati wa kushughulikia kesi za uchaguzi. Hukumu zisizo za haki huhatarisha umoja, mshikamano, amani na utulivu katika jamii.

**WAJIBU VIONGOZI WA VYAMA**

Viongozi wa vyama vya siasa wanapaswa kutambua kuwa wamebeba dhamana kubwa katika nchi, hivyo, waelewe wana wajibu mkubwa wa kuzuia ndimi zao kutoa kauli za uchochezi zenye kusababisha mpasuko na vurugu katika jamii. Wananchi wanayo shauku kubwa ya kusikia hoja za ilani za vyama zenye mwelekeo wa kujenga nchi na kutatua matatizo yao.

Kutenda haki ili kutunza amani na utulivu nchini ni wajibu wa kila Mtanzania, hivyo katika kuelekea uchaguzi mkuu, kila Mtanzania ana wajibu wa kuhakikisha unakuwa huru na haki huku amani na utulivu vikitamalaki. Yote hayo yanawezekana kila mmoja akitimiza wajibu wake.

Mwandishi wa makala hii ni Mchungaji wa KKKT, Mshauri, Mtafiti, Mwanataaluma na Mkurugenzi Mtendaji wa asasi isiyo ya Kiserikali ya Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare). Anapatikana kwa namba 0744 000066.

# Wakati pazia la kampeni likifunguka wagombea mnakumbuka mlikopita?



Baadhi ya wanasiasa na viongozi wamefikishwa kwenye Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi. **PICHA:MTANDAO.**

**Na Mwandishi Wetu**

PAZIA la kampeni za uchaguzi mkuu wa Oktoba 2020 lilifunguliwa Jumatano wiki iliyopita na sasa wagombea wanazunguka kila kona kuanzia mashariki hadi magharibi, kusini na kaskazini kuwafikia wapigakura.

Mengi yalijiri kwenye mchakato wa kupata wabunge na madiwani ikiwa ni pamoja na umati wa wagombea walikuwapo wasanii, wazee kwa vijana na viongozi mikoani, wilayani. Wajumbe kulaumiwa na lakini suala la 'kutoa kitu upate watu'.

Nipashe inazungumza katika mahojiano maalumu na mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam , Idara ya Sayansi ya Siasa na Utawala wa Umma, Sabatho Nyamsenda, kuchambua mchakato na kile cha kujifunza.....

**SWALI:** Watu waliotia nia katika nafasi za kuchaguliwa walikuwa wengi, mathalani CCM walikuwa zaidi ya 11,000, unadhani ni kwanini?

**JIBU:** Nadhani katika historia ya CCM, huu ndiyo uchaguzi pekee ambao wamejitokeza watu wengi kutia nia kwa ajili ya kuwania ubunge. Kwa mtazamo wangu, upo muunganiko uliosababisha idadi kubwa ya watia nia. Kwanza, wengi waliotia nia sio kwamba walitarajia kuwa watapita mchujo wa kura za maoni na kuteuliwa na chama chao, la hasha.

Wengi wamefanya hivyo kutokana na ukweli kwamba uteuzi serikalini baada ya uchaguzi wa 2015 ulikwenda kwa walioshindwa kura za maoni. Uteuzi wa mwanzo wa ukurugenzi wa halmashauri, ukatibu tawala wa wilaya na ukuu wa wilaya ulijazwa na watiania mwaka 2015.

Japo sijafanya utafiti wa kina kuhusiana na wasifu wa watia nia, nina uhakika kuwa wengi waliotia nia mwaka huu ni wahitimu au wanafunzi wa vyuo vikuu. Msukumo mkubwa ulikuwa ni kuonekana na mamlaka za uteuzi, wakitegemea kuwa hiyo itakuwa ndiyo tiketi ya kujipatia ajira na uteuzi mbali mbali.

Sababu nyingine ni wagombea wanaotaka kugombea kufanya hivyo kupitia chama wanachodhani wanaelekea

> Japo sijafanya utafiti wa kina kuhusiana na wasifu wa watia nia, nina uhakika kuwa wengi waliotia nia mwaka huu ni wahitimu au wanafunzi wa vyuo vikuu. Msukumo mkubwa ulikuwa ni kuonekana na mamlaka za uteuzi, wakitegemea kuwa hiyo itakuwa ndiyo tiketi ya kujipatia ajira na uteuzi mbali mbali.

kushinda, wengi ninaowafahamu walichukua kadi za CCM kati ya mwaka 2018 na 2020.

Pia, ni kweli kabisa kuwa umaarufu wa Mwenyekiti wa CCM, John Magufuli, hasa kutokana na mtindo wa siasa pendwa kumeongeza sana umashuhuri wa CCM na hivyo kuwavutia wengi.

**SWALI:** Je, kuna uwezekano wa kuvutiwa na maslahi manono ya kisiasa? Pengine kuna haja ya kubadilisha mifumo ya malipo ya wanasiasa?

**JIBU:** Bila kujali chama ambacho mgombea anajitokeza kuwania madaraka, sababu kubwa ambayo huwasukuma wanasiasa wengi kuamua kugombea nafasi za maamuzi ni malipo manono yanayotokana na nafasi hizo, pamoja na fursa zingine za kujitajirisha kupitia uhusiano na wafanya uamuzi au wafanyabiashara.

Mbali na kulipwa malipo maono yanayowaweka mbali na wapigakura wao, wanasiasa wengine wanatumia nafasi zao kujiingiza katika shughuli za kibiashara, wapo wanaotumia nafasi zao kushawishi kupata manufaa au hata kujipatia rasilimali za umma wakati mwingine kupitia ufisadi.

Kwa mfano, kuna wakati kashfa za ufisadi zilihusishwa na wanasiasa, baadhi yao wakiwa wabunge na mawaziri. Kuna muda zabuni nyingi za mabilioni katika ngazi ya halmashauri zilichukuliwa na kampuni zinazomilikiwa na madiwani na mameya.

Kwa hiyo, kubadilisha mfumo wa malipo ya wanasiasa kutasaidia kuleta mchujo ili wanaofanya siasa wawe ni watu wenye nia kuwatumikia wananchi.

Lakini, kubadili mfumo wa malipo peke yake hakutatosha. Kama nilivyosema hapo awali, wanasiasa wengi pia huingia katika nafasi hizo ili kupata urahisi wa kushiriki katika shughuli za kibiashara na mitandao ya ufisadi. Hivyo, utaona ni wazi kabisa tatizo lipo kwenye mfumo wa uchumi unaotilia mkazo ulimbikizaji binafsi wa mali. Mfumo huu unazalisha "wachumia tumbo" katika siasa. Kwa hiyo, kutenganisha siasa na biashara kutasaidia sana kupunguza wimbi hili la "wachumia tumbo" katika siasa. Lakini zaidi, kurekebisha mfumo wa uchumi ili faida inayozalishwa iende kutimiza mahitaji ya msingi ya walio wengi kutaliondoa kabisa tatizo la ulimbikizaji binafsi, na hivyo kukomesha tatizo la siasa za kuchumia tumbo.

**SWALI:** Kuna madai kuwa bila fedha hakuna kura za wajumbe, kama hutoi fedha hutapata kitu kwenye kura za kupendekeza watia nia. Je, usemi huo mwaka huu upo au umeondoka rasmi?

**JIBU:** Rafiki zangu zaidi ya 15 niliosoma ngazi mbalimbali za elimu walijitokeza kuwania nafasi za ubunge. Aliyechaguliwa ni mmoja mwenye uwezo kifedha. Wote niliozungumza nao walilalamikia kuwa, "bila kuwa na fedha hakuna anayekusikiliza". Kwa mujibu wa maelezo yao, hata mgombea akiwa na sera nzuri za kupita kiasi, alimradi hana fedha hawezi kuchaguliwa.

Kwa hiyo, usemi huo bado upo. Zipo semi nyingine kama, "mkono mtupu haulambwi" au "penye uzia penyeza rupia." Semi hizo huwa ni kiashiria cha fikra zinazotawala katika jamii. Fikra zilizotamalaki katika jamii, mara nyingi, hutengenezwa kwa lengo la kuhalalisha uhusiano wa kiuchumi uliopo katika jamii.

Mfumo wa kiuchumi wa ubepari wa gulio (neoliberalism) unaotawala zama hizi hugeuza kila kitu kuwa bidhaa kikauzwa na kununuliwa sokoni. Kwa maana hiyo, hata uchaguzi pia hugeuzwa kuwa gulio la kisiasa, ambapo mwanasiasa ndiye mteja na mpigakura muuzaji. Bidhaa inayouzwa ni kura. Kwa maana hiyo, kura hupoteza thamani (use value) na kubakia kuwa bidhaa yenye bei (exchange value). Tatizo hili lipo ndani ya vyama vya siasa.

# KAMALA HARRIS

## Mwanamama anayebadili sura ya kampeni urais Marekani

Na Ani Jozeni



CHAMA cha Democratic nchini Marekani ambacho kina matumaini makubwa ya kumshinda Rais Donald Trump kinaelekea kupata nguvu mpya kisiasa kutokana na shangwe katika sekta tofauti za jamii na mfumo wa uchumi na siasa wanchi hiyo.

Ni kutokana na kumchagua au kumteua Seneta Kamala Harris, mwanamama aliyewahi kuwa mwendesha mashtaka mkuu jimbo la California na mjumbe wa Baraza la Senate kitaifa.

Alikuwa mmoja wa watia nia katika ngazi za awali za kumtafuta mgombea urais wa chama hicho, ambako aliendana na mgombea Joe Biden, masuala kadhaa, na kutofautiana kwingine

Seneta Harris anakuwa mwanamama wa kwanza mwenye asili ya Kiafrika na India kuingia kwenye kinyang'anyiro cha ugombea urais na alionyesha kuwa ana uwezo wa kuleta 'ari , nguvu na kasi mpya' katika kampeni hizo, kupunguza vikwazo kwa kampeni ya Biden katika maeneo kadhaa.

'Amewakata maini' wafuasi wa Trump wanaosema Biden hana ujasiri wowote katika masuala ya kutekeleza sheria, kwani rekodi ya Seneta Harris katika jimbo la California ilikuwa kali. Ni kali kiasi kwamba wengi kati ya wanaharakati waandamizi wa fukuto la 'Black Lives Matter' wanamwona ni mmoja wa 'wabaya' wao.

Kudhihirisha kuwa Seneta Harris alikuwa chaguo sahihi, wengi kati ya wale waliokuwa wanasita kutoa michango kwa kampeni ya Biden (ambayo hata hivyo inaipita kampeni ya Trump kwa kuchangisha fedha, ingawa yeye anazo nyingi tu za kwake binafsi) walijitutumua.

Ndani ya saa 24 kutoka itangazwe kuwa ameteuliwa, kiasi cha Dola milioni 26 (zaidi ya Sh. bilioni 55) kilipatikana katika michango na taarifa zinasema kuwa kati ya waliochanga wakati huo, 150,000 walikuwa wanachanga kwa mara ya kwanza.

### KUKUBALIKA

Seneta Harris ana mvuto kwa makundi yote mawili, upande wa Democratic na hata Republican.

Baadhi ya wachambuzi wa siasa wanasema kuwa wanawake katika chama cha Democratic kwa miaka mingi wamekuwa ndiyo kundi tiifu kwa chama hicho kuliko makundi mengine lakini hawajawahi kuingia kwa tiketi ya kugombea urais.

Ila baadhi walipuuza uteuzi huo wakisema 'kuwa wa kwanza' katika jambo hili au lile hakubadili chochote, kwani Barack Obama alikuwa rais wa kwanza wa Marekani mwenye asili ya Kiafrika na kwa mujibu wa uhakiki huo, hakuna kilichobadilika.

Ila hakuna ubishi kuwa makundi kadhaa ambayo hayakuwa yanavutiwa na mgombea Biden moja kwa moja sasa yana uhakika zaidi nini kitazingatiwa akiwa pamoja na Seneta Harris ana misimamo ya kati ya dhati.

Wako waliounga mkono uteuzi huo kwa sababu wanamwona bora zaidi au wa kimabadiliko zaidi ya Biden hasa katika masuala ya mazingira licha ya kutokuwa na mwelekeo wa mageuzi kama kwa 'Black Lives Matter,' aliwahi kumkosoa kwa nguvu Biden wakati wa mijadala ya watia nia chama cha Democratic.

Ilifikia mahali Trump akaandika kwenye 'tweet'moja kuwa Harris aliwahi kumtaja Biden kuwa ni 'mbaguzi,' lakini wachambuzi wanasema Harris hakuwahi kutumia neno hilo, kuwa Trump aliongeza chumvi.

Wachamnbuzi wanasema katika kampeni yake kama mtia nia hatua ya kwanza ya kupata mgombea, Harris aliweka kipaumbele cha dhati suala la mazingira, zaidi ya Biden.

Ina maana uteuzi wake ni furaha kwa wale wanaotazamia kuona serikali yenye uwezo wa kupambana na maslahi ya 'big oil,'kampuni kubwa za mafuta nchini humo ambazo sasa zinafunguliwa milango kuingia katika hifadhi, za kimazingira au viumbe, kuchimba mafuta.

> "Seneta Harris anakuwa mwanamama wa kwanza mwenye asili ya Kiafrika na India kuingia kwenye kinyang'anyiro cha ugombea urais na alionyesha kuwa ana uwezo wa kuleta 'ari , nguvu na kasi mpya' katika kampeni hizo, kupunguza vikwazo kwa kampeni ya Biden katika maeneo kadhaa.

### KINACHOMWINUA

Mmoja wa wachambuzi anasema kuwa licha ya kampeni ya Harris kutafuta kupewa nafasi ya kugombea urais ilizimika mapema lakini inawezekana akafanya vyema zaidi akishindana katika kampeni na Republican kuliko alipokuwa akizozana na Democratic wenzake.

Isitoshe, wengi kati ya wapiga kura wenye asili ya Kiafrika (au Kihindi ambao kimsingi ni kundi moja) waliokuwa hawamweki maanani akiwa mtia nia sasa wanamwangalia katika sura tofauti.

Kiasi cha wanachama, wafuasi tisa kati ya 10 wa Democratic waliunga mkono kuteuliwa kwake.

Zaidi ya hayo, baadhi ya wafuatiliaji wa maoni wanasema anavutia wapiga kura wanawake kuliko Biden, pamoja na vijana wanaoanza kupiga kura au kwa mara ya pili, na anapendwa na baadhi ya wafuasi wa chama cha Republican.

Uteuzi huo pia unawapa nguvu wanasiasa wanawake jamii ya wenye asili ya Afrika au ya Kihindi wanaohitaji matumaini ya kupanda ngazi katika siasa za Marekani, kuwa siyo ajabu wakaanza kukubalika au kukubalika zaidi.

Uteuzi wa mwanamama huyo unaashiria kuwa na mwanamke mwemye asili ya jamii hizo isiwe jambo la kushangaza, hivyo kundi hilo lifaulu zaidi kwenye uchaguzi wa ngazi zote.

Kampeni ya Trump, kama wachambuzi walivyotazamia, ilijitahidi kumchora Harris kama mwanamageuzi asiyeaminika.

Hata hivyo, wengi kati ya wafuasi wa Republican waliomchoka Rais Trump wanahisi wamepata jibu .





# Waganga tiba asilia watakiwa kuchangamkia fursa viwanda

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imewataka waganga wa tiba asilia na tiba mbadala kuitumia fursa ya Tanzania ya viwanda kwa kuanzisha viwanda vidogo vya kuchakata dawa zitakazouzwa ndani na nje ya nchi, ili kuongeza pato la taifa kupitia sekta hiyo.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Prof. Mabula Mchembe, alisema hayo jana wakati wa ufunguzi wa maadhimisho ya Siku ya Tiba Asilia ya Mwafrika katika viwanja vya Nyerere Square, jijini hapa.

Alisema, waganga wa tiba asili wanatakiwa kuitumia fursa hiyo kwa kuanzisha viwanda vidogo vitakavyokuwa na uwezo wa kuchakata dawa zenye viwango.

Prof. Mchembe alisema kwa kutumia viwanda vidogo, waganga hao watazalisha dawa nyingi na zenye viwango ili kuziuza ndani ya nchi na nje.

"Waganga wanatakiwa kuanzisha viwanda vidogo vya kuchakata dawa za tiba asili pamoja na ile mbadala ili kupata soko la nje ya nchi, kujikwamua kiuchumi na kuongeza pato la taifa," alisema.

**Mpaka hivi sasa toka baraza hili lianzishwe, mmesajili dawa 30 pekee kiasi ambacho hakiridhishi. Ukilinganisha na uhalisia watu, bado wazalisha dawa nyingi sana huko mtaani.**

Aliliagiza Baraza la Taifa la Tiba Asili na Tiba Mbadala kuongeza jitihada katika kusajili dawa zinazotengezwa na waganga nchini.

"Mpaka hivi sasa toka baraza hili lianzishwe, mmesajili dawa 30 pekee kiasi ambacho hakiridhishi. Ukilinganisha na uhalisia watu, bado wazalisha dawa nyingi sana huko mtaani," alisema.

Pia aliwataka waganga hao kushirikiana na wataalamu wengine wa tiba ya kisasa katika kuboresha huduma zao.

"Waganga wanatakiwa kushirikiana na wataalamu wengine kama vile wafamasia na madaktari na wengine kuboresha huduma zao kuwa za kisasa ili kukuza sekta hii ya tiba asilia na tiba mbadala," alieleza.

Kadhalika, aliwataka waganga kufuata sera, kanuni na sheria za nchi kwa kuacha tabia ya kubandika matangazo yao katika nguzo za umeme katika maeneo mbalimbali ya nchi na yale ya kwenye vyombo vya habari lazima yawe na vibali.

"Lakini tabia nyingine ambayo naitaka muache waganga wengi mmekuwa waongo. Wengi wenu mnatumia dawa za kisasa mnazonunua katika maduka ya dawa na kuwapatia watu kwa kuchanganya na vitu vingine wakati si tiba asilia," alisema.

Katibu mkuu huyo pia aliwataka waganga wote, wasaidizi wao na vituo vyao vya kutolea huduma visajiliwe kinyume cha hapo wasitoe huduma.

Mkurugenzi wa Tiba katika Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Grace Magembe, alisema toka kuanzishwa kwa baraza la tiba asili na tiba mbadala nchini mwaka 2005, watumiaji wameongezeka.

"Tiba mbadala watumiaji wameongezeka hasa katika kipindi cha mapambano dhidi ya virusi vya corona nchini mwaka huu," alisema Magembe.



Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mabula Nchembe (mwenye miwani), akipata maelezo kutoka kwa mwakilishi wa kampuni ya utengenezaji wa dawa za tiba asili ya Shekilindi Bosnia, Bashiru Iddi (kulia), alipotembelea banda hilo kwenye maadhimisho ya Siku ya Tiba ya Asili Bora ya Mwafrika yanayofanyika kwa siku nne kwenye viwanja vya Mwalimu Nyerere, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Kampuni yawatangazia neema wakulima zabibu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAMPUNI ya Tanzania Distilleries Limited (TDL), imesema inatarajia kuingia mikataba ya moja kwa moja ya kununua zabibu kutoka kwa wakulima wadogo ikiwa ni dhamira yake ya kuendeleza kilimo cha zabibu mkoani Dodoma.

Akizungumzia mikakati ya kampuni hiyo kukuza kilimo hicho, Meneja Mkuu wa TDL, Davis Deogratius, alisema kampuni hiyo kwa sasa inanunua takribani lita milioni 1.2 za mchuzi wa zabibu kwa mwaka kutoka kampuni za CETAWICO na UWAZAMAM.

Deogratius alisema kampuni hizo zinanunua zabibu za wakulima wa ndani ambapo inatumia Sh. bilioni 3.3 kwa mwaka.

Alisema kampuni hiyo imedhamiria kununua malighafi zinazozalishwa ndani ya nchi katika kipindi chote cha miaka ijayo.

"Kwa sasa tunatumia malighafi na huduma za kufanikisha uzalishaji kwa asilimia 80 ambayo ni sawa na Sh. bilioni 46," alisema.

Aidha, alisema TDL imewekeza katika uundaji wa chapa za Kitanzania kwenye bidhaa za vinywaji kama vile mvinyo wa Imagi, Valeur, Wines Dodoma, Dodoma Rose, Konyagi na Zanzi Cream liqueur ambazo zimetengenezwa kwa viwango vya ubora wa kimataifa kwa kulenga mahitaji ya makundi mbalimbali katika soko.

"Mchango wa TDL wa sera yake ya kununua malighafi nchini una dhamira ya kukuza sekta ya kilimo cha zabibu ili iende sambamba na jitihada za serikali za kuboresha maisha ya wakulima wadogo na kukuza uchumi wa Tanzania," alisema.

Meneja huyo alisema TDL inaamini jitihada za serikali za kuigeuza Tanzania kuwa nchi ya viwanda zinafanikiwa ikiwa ni pamoja na wakulima wadogo kuwezeshwa kuzalisha malighafi inayohitajiwa na viwanda.

# Ujenzi hospitali, vituo vya afya wapunguza vifo mama, watoto

**Na Renatha Msungu,** KONGWA

KUJENGWA kwa Hospitali ya Wilaya ya Kongwa na vituo vya afya vinne, kimepunguza tatizo la wakazi wa wilaya hiyo kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya, imeelezwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, Dk. Omary Mkulo, alisema hayo jana alipokuwa akieleza utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika wilaya hiyo.

Alisema wakazi wengi walikuwa wakitembea umbali mrefu na wengine kupoteza maisha kutokana na huduma za afya kutokuwa karibu na maeneo yao.

"Tunaishukuru serikali kwa kujali sekta ya afya na siye tunailinda na kuiendeleza," alisema Dk. Mkulo.

Katika mwaka wa fedha 2019/20, alibainisha kuwa halmashauri ilipewa zaidi ya Sh. bilioni mbili kwa ajili ya kujenga hospitali ya wilaya, vituo vya afya pamoja na vifaa tiba.

Alisema vituo vipya vilivyojengwa ni pamoja na Mlali na Ugogoni na kwa sasa wanaendelea na ujenzi wa vituo vya afya vya Mbande na Mkoka.

"Tunamshukuru Rais wetu John Magufuli kwani tumepokea Sh. milioni 400 kwa ajili ya vituo vya Ugogoni, Mlali. Tunaendelea na ujenzi kwa ajili ya kituo cha afya cha Mbande. Rais Magufuli mwaka 2019 aliahidi kutoa Sh. milioni 100 lakini ametoa Sh. milioni 400 na ujenzi wake uko kwa asilimia 95. Pia tumepokea Sh. milioni 200 kwa ajili ya kituo cha Mkoka," alisema Dk. Mkulo.

Pia alisema zahanati 18 zimejengwa zikiwa na wodi ya mama na mtoto hali ambayo imepunguza vifo vya mama na mtoto.

Hata hivyo, alisema bado wanakabiliwa na tatizo la uhaba wa madaktari na wauguzi wa sekta ya afya.

Katika hatua nyingine, mkurugenzi huyo alisema halmashauri hiyo imetoa mikopo ya zaidi ya Sh. milioni 119 kwa vikundi 325 vya kinamama, vijana na walemavu.

Alisema licha ya utoaji wa fedha hizo kuna tatizo la vijana kutokurejesha mikopo kwa wakati, huku akiwasifia kinamama kurejesha kwa wakati.

"Vijana ni wachache ambao ni waaminifu, lakini kuna kikundi cha vijana wanakiwanda cha maziwa ambacho kinafanya kazi na tumewapa Sh. milioni 65," alisema Dk. Mkulo.





# Vijana wafurahia manufaa ubunifu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

**Zaidi ya vijana 300 katika Jiji la Mbeya wamejengewa uwezo wa kazi za mikono kupitia mradi wa kuwawezesha vijana ambao ulitekelezwa na kwa kushirikiana na FCS.**

BAADHI ya vijana kutoka Jiji la Mbeya wameanza kunufaika na ubunifu na kazi za mikono za utengenezaji wa bidhaa mbalimbali zinatokana na malighafi ambazo zinazalishwa nchini.

Wakizungumza na Nipashe jana katika maeneo wanakofanyia shughuli zao, walisema ubunifu wao si tu kwamba umeanza kutimiza malengo yao na kuwa chachu katika kuongeza kipato chao, bali umeongeza fursa za ajira kwa vijana wenzao na kuchangia katika uchumi wa nchi.

Joyce Chavala, mkazi wa Isyesye jijini Mbeya, ambaye amejiajiri kwa kutengeneza bidhaa mbalimbali zikiwamo sabuni na mikoba, alisema alianzisha mradi huo baada ya kupata mafunzo ya stadi za maisha kutoka taasisi zinazosaidia vijana na amekuwa akithubutu kutafsiri maarifa hayo kwa vitendo.

"Nalishukuru Shirika la Shop kwa kushirikiana na Foundation for Civil Society (FCS) kunipatia mafunzo ya kujitambua na ujasiriamali ambayo yamenisaidia kujiajiri kwa kuanzisha kiwanda changu kidogo cha kutengeneza sabuni na sasa nimeajiri na vijana wenzangu. Hakika nimeona mafanikio kwangu na familia yangu kwani sikuwa hivi awali," alisema Chavala.

Upendo Yohana, mkazi wa Ilemi, ambaye anatengeneza mazulia, alisema Tanzania ina fursa nyingi ambazo zitachochea mabadiliko chanya kwa vijana wenye uthubutu wa kufanya kazi kwa ajili ya maendeleo kuanzia ngazi ya kaya hadi taifa.

Mratibu wa Shirika la SHOP, Maria Dominick, alisema shirika hilo ni moja ya asasi zisizo za kiserikali zinazosaidia kuunga mkono jitihada za vijana kujikwamua kiuchumi.

Mbali na kuwasaidia vijana, pia alisema hufanya kazi kama njia ya kusaidia makundi ya vijana kubuni fursa za ajira ili kupungua utegemezi.

Alisema zaidi ya vijana 300 katika Jiji la Mbeya wamejengewa uwezo wa kazi za mikono kupitia mradi wa kuwawezesha vijana ambao ulitekelezwa na kwa kushirikiana na FCS.

"Uthubutu wa vijana hawa si tu kwamba unawanufaisha wenyewe bali unasaidia kupunguza changamoto za maisha hata kwa vijana wenzao ambao sasa wanapata fursa za ajira zisizo rasmi kupitia miradi inayobuniwa," alisema Dominick.



Mjasiriamali Joyce Chavala (kushoto), ambaye ni mkazi wa eneo la Isyesye, katika Jiji la Mbeya, akionyesha bidhaa zake za sabuni jijini humo jana, ambazo anazitengeneza baada ya kupata mafunzo kutoka Shirika la SHOP kwa kushirikiana na asasi ya Foundation for Civil Society (FCS). **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Waomba msaada kumalizia ujenzi kituo afya

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WANANCHI wa vijiji vitatu vya Kata ya Ilungu, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameiomba serikali na wadau wengine wa maendeleo kuwasaidia kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya walichoanza kujenga kwa nguvu zao.

Wamesema kukamilika kwa kazi hiyo kutawaepusha na madhara ya kusafiri umbali wa zaidi ya kilometa 80 kufuata huduma za afya katika Hospitali Teule ya Wilaya ya Ifisi.

Kwa mujibu wa wananchi hao walipozungumza jana na Nipashe, walisema wanaomba wadau na serikali kuwaunga mkono kukamilisha kituo hicho ili kuondokana na adha hiyo ya muda mrefu.

Wananchi hao ambao wanatoka vijiji vya Shango, Mwela na Kikondo, waliamua kuanza ujenzi wa kituo cha afya katika kijiji cha Shango baada ya kukumbwa na shida kubwa ya upatikanaji wa huduma za afya hasa kwa wajawazito na watoto.

Mmoja wa wananchi hao, Mwansele Bhilagu, kutoka Shango, alisema vijana ambao ni nguvu kazi walijitahidi kujitoa kujenga jengo hilo kwa kufyatua matofali na kupasua mbao.

Alisema kutokamilika kwa ujenzi wa kituo hicho, kunasababisha waendelee kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za matibabu katika Hospitali ya Ikonda iliyoko wilayani Makete, ambapo ni takribani kilometa 200 pamoja na ile ya Ifisi.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Shango, Petro Mwala, alisema mbali na wananchi hao kujitolea nguvu zao, pia wamekuwa wakitoa michango ya fedha na mali zao kwa ajili ya ujenzi na kwamba sasa wanahitaji msaada wa kumalizia kazi hiyo.

"Tunahitaji nguvu ya wadau na serikali kukamilisha ujenzi huu. Tulipofikia pamoja matumaini tumejitahidi sana kinamama walikesha kubeba matofali, vijana nao walisaidia, sasa kilichobaki ni umaliziaji," alisema Mwala.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Shango, Emily Mwakalila, alisema hadi sasa wananchi hao wameshatumia zaidi ya Sh. milioni 150 kutekeleza mradi huo.

## Madereva wa mabasi waonywa utupaji taka

**Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (Latra) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, imesema inafanya ufuatiliaji wa madereva na makondakta wa mabasi ya mikoani kwa kutumia mfumo wa ufuatiliaji mienendo ya mabasi (VCT) ili kubaini wanaokiuka sheria za usafi wa mazingira kwa kutupa taka ovyo.

Meneja wa LATRA wa kanda hiyo, Denis Daudi, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Daudi alisema licha ya kutoa katazo na madereva kutunza mazingira kwa kutotupa taka barabarani, bado baadhi wanaendelea na kwamba kazi hiyo sasa itasimamiwa ipasavyo.

Alisema wamelazimika kutumia mfumo huo baada ya uchafuzi wa mazingira kuendelea kufanywa na madereva husussani wa malori na mabasi makubwa.

"Tumebaini pia baadhi ya makondakta huwa wanatupa taka kwenye maeneo ambayo hayajatengwa kwa ajili ya shughuli hiyo licha ya kuelekezwa maeneo maalumu ya kutupa taka. Utupaji ovyo wa taka hizo unaweza ukasababisha magonjwa ya mlipuko na kuwadhuru baadhi ya wanyama, hivyo ni lazima udhibitiwe kwa nguvu zote," alisema Daudi.

Daudi aliwataka wamiliki wa mabasi kukaa na kuzungumza na makondakta na madereva ili wafuate maelekezo wanayoyapata kutoka idara za serikali na kwamba katika mkoa wa Mbeya tatizo hilo lilikuwa katika eneo la Igawa wilayani Mbarali.

Baadhi ya wananchi waliviomba vyombo mbalimbali vya serikali vinavyohusika na shughuli za usafirishaji kusaidia kudhibiti utupaji ovyo wa taka kwenye maeneo mbalimbali.

Justin Alinikisa, dereva daladala jijini Mbeya, alisema ni muhimu vyombo vya usafiri vikazingatia usafi ili kujiepusha na magonjwa ya mlipuko, lakini kuzingatia sheria, LATRA inataka na kwamba makondakta wakorofi ambao wanakaidi agizo hilo wachukuliwe hatua.

Baadhi ya abiria walisema wao ni miongoni mwa wanaosababisha uchafuzi wa mazingira kwa kutotumia vifaa vilivyo ndani ya magari kuhifadhia taka zao badala yake hutupa barabarani.





# Kero ununuzi umeme kisa mtandao

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

HUDUMA ya kununua umeme Zanzibar imesababisha adha ya watu kupanga foleni kubwa kutokana na mfumo wa ununuzi kupitia mtandao wa simu kuwa na hitilafu.

Kutokana na hali hiyo, baadhi ya wananchi wameliomba Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kurudisha huduma ya ununuaji wa umeme kupitia mtandao wa simu ya mkononi ZANTEL ili kuokoa muda wa kupanga foleni katika vituo vya kununua umeme.

Wakizungumza na Nipashe jana, baadhi ya wananchi hao walisema kukosekana kwa huduma hiyo ya kununua umeme kwa njia ya mtandao, kumesababaisha kuwapo kwa foleni kubwa ya watu wanaohitaji nishati hiyo katika vituo vya umeme.

**Wateja wote watakaofika kwenye vituo vya kuuzia umeme watahudumiwa ili kuhakikisha wanapata huduma hiyo bila ya kukosa.**

Mussa Omar, mmoja wa wananchi hao, alisema huduma ya kununua umeme wa mtandao wa simu unarahisisha muda, hivyo ni vyema shirika hilo likarejesha huduma hiyo kwa haraka.

"Tokea saa 10: 00 jioni nimepanga foleni ya kununua umeme katika kituo hiki cha Mazizini na hadi sasa saa moja usiku bado sijafanikiwa," alisema.

Mussa alisema baadhi ya shughuli zake za kijamii zimesimama kutokana na kutokuwa na umeme hali ambayo imemlazimu kutumia muda mwingi wa kutafuta huduma hiyo.

Ofisa Uhusiano wa ZECO, Salum Abdallah, aliwataka wananchi wa Zanzibar kutumia vituo vya kununua umeme kutokana na kukosekana kwa huduma ya kununua kupitia njia ya mtandao ya simu za mkononi ya ZANTEL wa Ezy Pesa.

Alisema kwa sasa huduma ya kununua umeme kwa njia ya simu kupitia Ezy Pesa pekee ndio imesimama kufanya kazi tangu juzi kutokana na matatizo yaliyojitokeza kupitia mfumo huo.

"Wateja wote watakaofika kwenye vituo vya kuuzia umeme watahudumiwa ili kuhakikisha wanapata huduma hiyo bila ya kukosa," alisema.

Aidha, alisema Shirika kwa sasa linashirikiana na mtandao wa simu wa ZANTEL ili kuhakikisha tatizo hilo linatatuliwa na kuwaondolea usumbufu wananchi katika kujipatia huduma hiyo.

Tokea juzi vituo vya kuuzia Visiwani Zanzibar vimekuwa na foleni kubwa ya wananchi wanaohitaji huduma hiyo.

# Mgombea urais CUF rasmi leo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA wa urais wa Zanzibar kupitia chama cha CUF, Mussa Haji Kombo, leo anatarajiwa kuchukua fomu fomu kuwania nafasi ya urais wa Zanzibar, katika Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC).

Wakati mgombea huyo akitarajiwa kufanya hivyo, uongozi wa chama hicho umelaani vikali kauli za mgombea urais wa ACT-Wazalendo, Maalim seif Sharif Hamad, zinazodaiwa kuwa na mwelekeo wa kuhamasisha vurugu za kisiasa kuelekea uchaguzi mkuu.

Akizungumza jana na waandishi wa habari mjini Zanzibar, Kombo alisema wataingia katika kinyang'anyiro cha urais wa Zanzibar na kuahidi kulinda amani na utulivu na kuepuka vurugu zinazoweza kusababisha wananchi kuishi katika maisha ya dhiki.


"Ndugu waandishi wa habari natangaza rasmi nakusudia kuchukua fomu kuwania nafasi ya urais wa Zanzibar kwa tiketi ya CUF. Wapo watu walikuwa wakisema kwamba tumeyumba si kweli bado tupo imara," alisema.

Kombo ambaye ni miongoni mwa waanzilishi wa CUF, aliwataka wananchi kupuuza kauli za vitisho za kuwataka vijana kukaa tayari kukabiliana na dola kwa kile alichodai vitendo vya uonevu kwa wagombea wa chama hicho kuwekewa pingamizi katika majimbo ya uchaguzi yaliyopo Pemba.

Alisema wananchi wa Pemba bado hawajasahau watu waliopoteza maisha yao kwa sababu za vurugu za kisiasa za mwaka 2001 na wengine kuwa wakimbizi Mombasa, Kenya ambazo kwa kiasi kikubwa zilisababishwa na kiongozi huyo kupinga matokeo ya uchaguzi mkuu.

Alisema suala la kuwekewa pingamizi sio la kwanza na chama hicho kiliwahi kuwekewa pingamizi na NCCR Mageuzi na kupoteza majimbo sita Pemba lakini hakukuwa na kauli za aina hiyo zinazoashiria vurugu za kisiasa.

Aidha alivitaka vyombo vya dola na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuzifanyia kazi kauli hizo na zikiachiwa zinaweza kuathiri maendeleo ya uchaguzi na kuwatisha wananchi kushindwa kutumia haki ya kidemokrasia.



Ofisa Elimu kwa Umma wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi (ZAECA), Mkoa wa Kaskazini Pemba, Kassim Yussuf Ali, akizungumza na wananchi wa Madenjani, kuhusu suala la rushwa kuelekea uchaguzi mkuu katika mkutano ulioandaliwa na Shirika la Actionaid Pemba. **PICHA: ZUHURA JUMA**

# Mji wa Zanzibar kung'arishwa kwa taa za umeme

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar, Khamis Mussa, amesema lengo la serikali kuweka taa za kisasa za barabarani ni kuweka mji wa Zanzibar katika haiba nzuri na kuimarisha usalama wa wananchi.

Aliyasema hayo baada ya hafla ya utiaji saini mkataba wa makabidhiano ya mradi wa uwekaji taa za kisasa wa awamu ya pili katika mkoa wa Mjini Magharibi. Hafla hiyo ilifanyika katika Shule ya Sekondari Lumumba.

Khamis alisema baadhi ya madereva wamekuwa wakizifanyia hujuma taa hizo kwa kuzivunja kwa makusudi bila kujali serikali imetumia fedha nyingi katika kuziweka.

Alisema miundombinu hiyo iliwekezwa kwa fedha nyingi kwa ajili ya usalama wa wananchi na wageni wanaoingia nchini, hivyo si vyema kuihujumu kwa makusudi.

Akizitaja barabara zilizowekewa miundombinu hiyo ni za Mkapa kutoka Amani hadi Mtoni na Malawi kutoka Malindi hadi kwa Nyanya.

Kutokana na uwekezaji huo, aliwaomba madereva na wananchi kuitunza miundombinu hiyo ili kutorejea kutumia fedha nyengine kuweka taa hizo ambazo zinawezekana kutunzwa kwa muda mrefu.

Hata hivyo, alieleza kwamba serikali itaangalia uwezo wa kiuchumi ili kuweka taa hizo katika barabara za vijijini.

Katibu huyo aliipongeza serikali ya watu wa China kuendelea kuisaidia Zanzibar katika miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa hospitali ya Abdalla Mzee kisiwani Pemba.

Naye Balozi Mdogo wa China aliyekuwapo Zanzibar, Xie Xiao Wu, alisema serikali ya China itaendelea kuisaidia Zanzibar hasa katika shughuli mbalimbali za kijamii.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ anayeshughulikia Serikali za Mitaa, Khalid Abdalla Omar, akitoa maelezo ya kitaalamu, alisema mradi huo umejumuisha shughuli mbalimbali ikiwamo ukarabati wa taa katika mradi wa kwanza katika eneo la Michenzani na Darajani kwa kuweka waya wa umeme zenye urefu wa kilomita 4.5, kubalidisha betri chakavu za nguvu ya jua vifaa vya kuwasha taa na kuweka taa mpya 131.

Alisema mradi huo ulikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kukatika kwa waya kwa kamera za usalama, uharibifu wa nguzo zinazogongwa na gari na ukataji wa barabara katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya uwekaji wa waya za umeme.

Mradi wa uwekaji wa taa za barabarani kwa awamu ya pili umeanza ujenzi Novemba 28, 2018 na kukamilika Febuari, mwaka huu na kugharimu Sh. bilioni 8.5.

# MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**KIWANJA KINAUZWA, K**IWANJA CHA COMMERCIAL 1300SQM KINAUZWA KIPO REGENT ESTATE HAKUNA DALALI TUPIGIE: 0693 689996/ 0757 129546

**KIWANJA KINAUZWA,** Kipo ukonga kitunda Mwanagati Ukubwa 3175sqm kandoni mwa barabara kubwa kimepimwa kinafaa kwa shughuli yeyote utakayo ujirani mzuri, Lorry kubwa kinaingia Bei ni 75 mil. Mawasiliano: 0719 619 444/ 0782 574 669


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA CHETI



115880702

**Dainess Milkel Malisa** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0750/0528** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Tanzania mwaka 2016 katika Shule ya Sekondari Oshara. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **URP/RB/4421/2020**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JOHN JOACHIM MAKABE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0168/0507** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia St. Joseph Seminary Sanu mwaka 2001. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **SIN/SIN/RB/630553/2020.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO (W)-BOMANI WILAYA YA IRINGA**

**SHAURI LA MADAI YA TALAKA 16/2020**

**JENIFA ALFONSI MNYAGALAH.................MDAI**

**DHIDI YA**

**ABUBAKARI A. NGA'MILO .............MDAIWA**

**KUITWA SHAURINI**

Shauri la madai ya Talaka tajwa hapo juu limefunguliwa katika Mahakama hii, na mdai dhidi yako mdaiwa.

Hivyo unaamriwa wewe mdaiwa popote pale ulipo kuhudhuria hapa Mahakamani tarehe 9/9/2020 saa 2:30 asubuhi bila kukosa kwa ajili ya kujibu madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikiliza shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako kwa ajili ya kujitetea.

Usipofika bila taarifa shauri litasikilizwa upande mmoja na hukumu kutolewa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 11/8/2020.

MAHAKAMA YA MWANZO BOMANI

IRINGA.

115881702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

**Katika mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa mirathi 50/1989**

**Ombi la TARANGE SALEHE kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu MWANAIMA HANDA DIGO**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA.**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe16/09/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 01/9/2020

URBAN DODOMA

115882702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;250/2020**

**Ombi la VICTORIA KALANJE MAVURA,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ABDALLAH MOHAMED MAVURA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 07/09/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 01/09/2020.

Sahihi ya Hakimu

115882602

## KUPOTEA KWA CHETI



115878502

**Kelvin Robert** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0731-0396** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Tanzania mwaka 2011 katika Shule ya Sekondari Makongo. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **Ref: KAWE/2020**

## KUPOTEA KWA CHETI



115881902

**Nancyninah A. Joseph** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1197/0081** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Tanzania mwaka 2009 katika Shule ya Sekondari Green Acre. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **Ref: KAWE/2020**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;249/2020**

**Ombi la HAPPYFANIA AUGUSTINO MOSHA,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu THERESIA EDWARD MUNIO.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 29/09/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 01/09/2020.

115882502

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GERALD JOHN KIHINGA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA MARK II YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 626 BDH.** YENYE CHASSIS NO. **GX1006167684.** KWA YOYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.
TAARIFA YA POLISI: **DAR/BUG/RB/634207/2020.**

115882202

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**VIOLETA GODFREY MNZAVA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA NOAH YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 206 DCX.** YENYE CHASSIS NO. **AZR600430482** NA ENGINE **NO. 1AZ5182870.** KWA YOYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.
TAARIFA YA POLISI: **DAR/MBA/RB/630383/2020.**

115881202

## KUPOTEA KWA CHETI



115882002

**MOSHI M. KIMIZI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P.320/9** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Kigoma S/S Centre Novemba 1985. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. **DSM/PHQ/RB/633134/2020.**


Uza,

Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi

Kwa Bei Poa

Tupigie 0782253676

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Watoto 70,000 hatarini kufa

**LONDON, Uingereza**

SHIRIKA la Kimataifa linalohusika na watoto la Save the Children, limeonya kwamba watoto 70,000 katika eneo la Jangwa la Sahara wanakabiliwa na tishio la kufariki dunia kutokana na njaa kabla ya mwisho wa mwaka huu.

Shirika hilo pia linasema janga la corona limezifanya baadhi ya familia kushindwa kukidhi mahitaji yao ya msingi.

Kufikia sasa shirika hilo linasema idadi ya watoto wanaokabiliwa na utapiamlo imeongezeka hasa katika maeneo ya Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Save The Children limeongeza kuwa amri ya kutotoka nje ilizifanya familia nyingi katika bara la Afrika kupoteza njia za kujikimu.

Kwa mujibu wa uchunguzi wake zaidi ya watoto 67,000 huenda wakapoteza maisha yao kutokana na changamoto hizo kufikia mwisho wa mwaka huu.

Tahadhari kama hiyo pia imetolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula Duniani likiangazia namna viwango vya ukosefu wa chakula vilivyopanda kutokana na janga la corona. ***BBC***



Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, ameamuru Wizara ya Afya kuchapisha zabuni zote zinazohusiana na namna serikali ilivyoshughulikia janga la corona. **PICHA: REUTERS**

# Kamanda wa juu jeshini atimuliwa madai rushwa

**RIYADH, Saud Arabia**

KAMANDA wa cheo cha juu wa Jeshi la Saudi Arabia, anayeongoza majeshi ya muungano yanayopigana nchini Yemen, pamoja na mtoto wake wa kiume wamefukuzwa kwa madai ya kuhusika na vitendo vya rushwa.

Kwa mujibu wa shirika la habari la serikali, SPA, Mfalme Salman wa Saudi Arabia ametoa amri ya kifalme jana kumuondoa Luteni Jenerali, Fahad bin Turki bin Abdulaziz.

Abdulaziz ni kamanda wa vikosi vya muungano katika vita nchini Yemen vinavyoongozwa na Saudi Arabia dhidi ya wana mgambo wa Houthi wanaoungwa mkono na Iran.

Likinukuu amri hiyo ya kifalme shirika hilo limesema Luteni Jenerali huyo amestaafishwa na amewekwa chini ya uchunguzi.

Mtoto wake wa kiume, Mwanamfalme Abdulaziz bin Fahad bin Turki bin Abdulaziz Al Saud, ambaye ni Naibu Gavana wa Jimbo la Al-Jouf, Kaskazini mwa Saudia, pia ametimuliwa na kuwekwa chini ya uchunguzi.

Nafasi ya kamanda Fahad imechukuliwa na Multaq bin Salim, Naibu Mnadhimu wa Jeshi, kutokana na mapendekezo ya mrithi mwanamfalme Mohammed bin Salman.

Kwa mujibu wa amri hiyo ya kifalme, uamuzi huo umetokana na pendekezo la mrithi mwanamfalme Mohammed bin Salman kufanya uchunguzi kuhusiana na shughuli za kifedha zilizotiliwa mashaka ambazo zilifuatiliwa katika wizara ya ulinzi.

Amri hiyo ya kifalme ilisema kwamba wakala wa kupambana na rushwa Nazaha ulifichua rushwa ya fedha katika wizara hiyo inayomhusisha baba na mtoto wake wa kiume na maofisa wengine wanne wa jeshi pia wanachungzwa kutokana na sakata hilo.

Mwezi Machi mwaka huu, Shirika la Kutetea Haki za Binadamu Human Rights Watch lilieleza wasiwasi wake kuhusu ukamataji wa maofisa 298 wa Saudi Arabia kwa madai ya kuhusika na vitendo vya rushwa. Shirika hilo lilionya kuhusu uwezekano wa kuendeshwa kesi zisizokuwa na haki katika taifa ambalo mfumo wake wa kimahakama hauko wazi.

Kwa mujibu wa wakala wa kupambana na rushwa wa Saudi Arabia, maofisa wa jeshi na idara ya mahakama walikuwa miongoni mwa waliotiwa mbaroni kwa madai ya kutoa au kupokea hongo na matumizi mabaya ya fedha za umma zinazofikia thamani ya jumla ya riyale milioni 379, ambazo ni sawa na dola milioni 101. ***DW***

## Wanamgambo Congo wadaiwa kubaka wanafunzi

**DRC, Congo**

WANAMGAMBO waliojihami wamevamia shule nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na kuwabaka wanafunzi wa kike mkesha wa mtihani.

Wanaume hao walivamia kituo kilichokuwa kinawahifadhi wanafunzi 35 waliokuwa wakisubiri kufanya mitihani yao ya mwisho wa mwaka katika mji wa Isiro, ambao ni makao makuu ya mkoa wa The Haut-Uélé.

Mamlaka katika eneo hilo zinasema baadhi ya wanafunzi walibakwa wakati wa shambulio hilo.

Wanafunzi walienda kufanya mtihani siku ya Jumatatu, kwa mujibu wa mchungaji katika eneo hilo.

Mamia ya wanafunzi wametoroka baada ya shambulio lingine kama hilo kuripotiwa katika kituo kingine cha mitihani, kulingana na shirika la habari la AFP.

Wanafunzi 700 na walimu wao walitoroka kutokana na shambulio hilo lililotokea karibu na mpaka wa Sudan Kusini.

Wanamgambo hao wanadai walikuwa wanataka kusambaratisha mitihani hiyo, kwa mujibu wa msemaji wa jeshi katika eneo hilo, Dieudonne Kasereka aliyenukuliwa na AFP. **BBC**

**Mamia ya wanafunzi wametoroka baada ya shambulio lingine kama hilo kuripotiwa katika kituo kingine cha mitihani, kulingana na shirika la habari la AFP.**

# Macron aishinikiza Lebanon kuunda serikali mpya

**BEIRUT, Lebanon**

RAIS wa Ufaransa, Emmanuel Macron, amerejea Lebanon, nchi ambayo kwa sasa ipo katikati ya mgogoro usio wa kawaida.

Marcon amerejea nchini humo kwa ziara ya siku mbili iliyosheheni shughuli nyingi na mazungumzo ya kisiasa yanayolenga kuipa ufumbuzi nchi hiyo.

Kiongozi huyo juzi usiku aliwasili mjini Beirut, lakini mkutano wake wa kwanza haukuwa na Waziri Mkuu mpya aliyeteuliwa saa chache kabla, wala wanasiasa wanaozozana wa nchi hiyo au wanaharakati wa mashirika ya kijamii.

Macron badala yake aliamua kumuona mwanamuziki nambari moja wa kike nchini Lebanon, Fairouz, ambaye ni alama ya kitaifa na mmoja wa vigogo wa nadra nchini Lebanon wanaopendwa na kuheshimiwa.

Mwanamuziki huyo maarufu katika ulimwengu wa Kiarabu, sasa ana umri wa miaka 86 na hajaonekana hadharani katika miaka ya karibuni.

Kisha akakutana na Waziri Mkuu wa zamani, Saad Hariri, katika makazi ya balozi wa Ufaransa.

Akizungumza katika uwanja wa ndege wa Beirut, Macron alitoa wito wa kuundwa haraka serikali mpya ya Lebanon kutokana na kuteuliwa kwa Waziri Mkuu mpya.

"Nimeona mchakato umeanza katika saa chache zilizopita ambao umewezesha kupatikana kwa Waziri Mkuu, siyo jukumu langu kumuidhinisha au kumbariki ni uhuru wa Walebanon ambao ndio suala la msingi hapa.

"Lakini, uhakikishe kuwa serikali yenye lengo inaundwa haraka iwezekanavyo ili kutekeleza mageuzi ambayo tunatambua kuwa yanahitajika kutoa huduma kwa Walebanon."

Macron aliwasili saa chache tu baada ya viongozi kumteua Mustapha Adib, mwanadiplomasia mwenye umri wa miaka 48, kuwa Waziri Mkuu mpya na mwenye jukumu la kuukabili mgogoro mkubwa wa nchi hiyo wa kisiasa na kiuchumi.

Rais Michel Aoun mwenye umri wa miaka 85 na mshirika wake wa kisiasa, kiongozi wa Hezbollah, Hassan Nasrallah, walieleza kuwa tayari kubadilisha namna Lebanon inavyoongozwa.

Macron alikuwa kiongozi wa kwanza wa kigeni kuitembelea Lebanon siku mbili baada ya mlipuko wa Beirut uliowaua watu 188 na kuwajeruhi maelfu ya wengine.

Aliahidi kurejea Septemba Mosi kushiriki katika matukio ya kuadhinimisha miaka 100 ya uhuru wa Lebanon kutoka kwa Ufaransa. ***DW***

# MESSI AKACHA MAZOEZI YA KWANZA BARCELONA




**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi hakuwa sehemu ya kikosi cha Barcelona kilichoanza mazoezi yake kwa mara ya kwanza chini ya kocha, Ronald Koeman wakati mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or akiendelea kuhimiza kutaka kuondoka hapo Camp Nou.

Messi aliushtua ulimwengu wa soka kwa kuiarifu Barca nia yake ya kutaka kuondoka wiki iliyopita.


Wakati kikosi hicho kilifanyiwa kwanza vipimo vya corona Jumapili kabla ya kuanza mazoezi na Koeman, Messi hakuhudhuria kwa sababu anaamini kifungo cha mkataba wake kinamruhusu kuondoka akiwa huru bado kinafanya kazi na maana yake kwamba sasa si mchezaji tena wa Barcelona.

Hali hiyo imezua taharuki kwa klabu na Ligi ya Hispania, LaLiga, ilitoa taarifa Jumapili kwamba, Messi bado kifungo chake cha kuondoka kwa euro milioni 700 hakijaisha muda wake.

Manchester City inayonolewa na kocha wa zamani wa Messi, Pep Guardiola imekuwa ikionekana kuwa mstari wa mbele kuwania saini yake.

Koeman ameripotiwa kuwaambia Luis Suarez na Arturo Vidal kwamba majaliwa yao hayapo ndani ya klabu hiyo na kwamba wanatakiwa kutafuta sehemu ya kwenda, lakini wote walikuwa kwenye mazoezi ya kikosi hicho kilichokuwa na wachezaji 19.

Ivan Rakitic aliruhusiwa kukosa mazoezi wakati akiwa anajiandaa kukamilisha mipango yake ya kurudi kwa mabingwa wa Ligi ya Europa,



## MKHITARYAN AJIUNGA JUMLA NA ROMA

**ROME, Italia**

HENRIKH Mkhitaryan amejiunga moja kwa moja AS Roma baada ya Arsenal kukubali kuvunja mkataba wake pale kwenye dimba la Emirates.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Armenia, alitumia msimu wa 2019-20 akiwa na miamba hao wa Serie A , akifunga mabao tisa katika mechi 2 7 kwenye mashindano yote.

Dili hilo lilikuwa linamalizi- ka mwisho-
ni Juni na alikubali kuongeza mkataba wa
muda mfupi baada ya ligi kuchelewa kumalizika
kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Mkhitaryan alihamia kwa Arsenal akitokea Man-
chester United, Janu- ari mwaka 2018 kama se-
hemu ya dili lililom- husisha Alexis Sanchez
kwenda upande mwingine.

Alifunga mabao tisa katika mechi 59 al-
izocheza kwenye mashindano yote kabla
ya kujiunga na Roma.

Taarifa ya Arse- nal kwenye tovuti yake ili-
someka: “Tume- kubaliana kuvunja mkataba
wake kwa maele- wano na kumruhusu kuji-
unga moja kwa moja Roma.

“Kila mmoja hapa Arsenal anamshukuru Micki
kwa mchango wake kwa klabu na tunamtakia
kila la heri kule AS Roma.”

## ZIYECH ATABIRIWA MAFANIKIO CHELSEA

**LONDON, England**

JESPER Olsen amesema “hakuna shaka” Hakim Ziyech atakuwa na mafanikio makubwa chini ya Kocha, Frank Lampard pale Chelsea baada ya kuondoka kwa miamba wa Uholanzi, Ajax.

Ziyech anajiandaa kuanza msimu wake wa kwanza kwenye Ligi Kuu baada ya kutua hapo Stamford Bridge kwa pauni milioni 33.3 akitokea Ajax, Julai mwaka huu.

Winga huyo raia wa Morocco, ambaye alitoa pasi za mwisho 10 katika mechi za mwisho sita kule Amsterdam, alionyesha kiwango cha kuvutia kwenye mchezo wake wa kwanza pale Chelsea wakati wakitoka sare ya 1-1 na Brighton and Hove Albion katika mchezo wa kirafiki wiki iliyopita.

Olsen, ambaye alishinda mara mbili mfululizo taji la Ligi Kuu Uholanzi, Eredivisie, na lile la KNVB wakati wa kipindi chake cha kwanza kule Ajax kati ya mwaka 1981 na 1984 kabla ya kujiunga na Manchester United, alikiambia kituo cha habari cha Stats Perform kuwa: “Hakuna shaka kwamba atakuwa na mafanikio pale Chelsea.

“Nafikiri Frank Lampard amefanya kazi nzuri sana. Anaijua klabu ndani na nje. Anaonekana kuwa vizuri sana kwenye suala la utawala na staili ya uchezaji.

“Hicho ni kitu muhimu, anataka kushambulia na kucheza soka la kujilinda. Hilo halitakuwa tatizo kwa Ziyech.

“Wachezaji wanaotoka Ajax, wanapenda hivyo. Kuwa mlinzi na kiungo. Hakuna shaka juu ya hilo.”



## HAVERTZ KIMEELEWEKA CHELSEA

**MUNICH, Ujerumani**

KOCHA wa Bayer Leverkusen, Peter Bosz hatarajii Kai Havertz kufanya tena mazoezi na klabu hiyo, wakati kiungo huyo akijiandaa kujiunga na Chelsea.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani imeripotiwa anatarajiwa kusaini na Blues hao kwa dili lenye thamani ya pauni milioni 72.

Havertz atakuwa mchezaji wa saba kusajiliwa na Chelsea kipindi hiki cha dirisha kubwa la usajili baada ya Timo Werner, Hakim Ziyech, Ben Chilwell, Thiago Silva, Malang Sarr na Xavier Mbuyamba kutua hapo kwenye dimba la Stamford Bridge.


Akizungumza na waandishi Jumatatu, Bosz alisema: “Bahati mbaya kikosi chetu bado hakijajulikana vizuri.

“Sitarajii Kevin Volland au Kai Havertz kufanya tena mazoezi na sisi. Inawezekana wachezaji wengine pia wataondoka.

“Tunatakiwa kuwaleta wachezaji wengine pia. Kwa kawaida maandalizi ya msimu yanachukua wiki sita, hivyo ni faida kwetu kwamba tunaweza kutafuta wengine.

“Litakuwa jambo kubwa kwa makocha kama kikosi kitakuwa kimekamilika kabla ya kuanza kwa mazoezi.”

Havertz alifunga mabao 19 katika mashindano yote msimu uliopita wakati Leverkusen ikimaliza nafasi ya tano kwenye msimamo wa Bundesliga, na ilifika robo fainali ya Ligi ya Europa na fainali ya Kombe la DFB-Pokal, ambapo walifungwa na Bayern Munich.



# GREALISH

## AITWA ENGLAND KWA MARA YA KWANZA

**LONDON, England**

KIUNGO wa Aston Villa, Jack Grealish ameitwa kwa mara ya kwanza kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya England kilichotajwa na kocha wake, Gareth Southgate.

Hata hivyo, Marcus Rashford na Harry Winks ambao ni majeruhi wametolewa katika kikosi hicho kinachojiandaa na mchezo dhidi ya Iceland na Denmark kwenye michuano ya Ligi ya Mataifa ya UEFA.

Grealish mwenye umri wa miaka 24, amewahi kuiwakilisha England katika timu ya wachezaji wa umri chini ya miaka 21 na alikuwa sehemu ya timu mwaka 2016.

Wachezaji wengine wapya walioitwa kwenye kikosi hicho ni Conor Coady wa Southampton na beki wa Arsenal, Ainsley Maitland-Niles.

Kikosi cha Southgate kitacheza dhidi ya Iceland hapo Jumamosi kabla ya kuivaa Denmark siku tatu baadaye.

Kikosi kamili

Makipa: Dean Henderson, Jordan Pickford na Nick Pope.

Walinzi: Trent Alexander-Arnold, Conor Coady, Eric Dier, Joe Gomez. Michael Keane, Ainsley Maitland-Niles, Tyrone Mings, Kieran Trippier na Kyle Walker.

Viungo: Phil Foden, Mason Mount, Kalvin Phillips, Declan Rice, James Ward-Prowse, na Jack Grealish.

Washambuliaji: Tammy Abraham, Mason Greenwood, Danny Ings, Harry Kane, Jadon Sancho, na Raheem Sterling.



## SILVA AJIPANGA KUZIPIKU BARCELONA, REAL MADRID

**MADRID, Hispania**

DAVID Silva amesema malengo yake ni kushinda taji na Real Sociedad baada ya kutua hapo akitokea Manchester City.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, ambaye alishinda mataji manne ya Ligi Kuu England, EFL mara tano na FA mara mbili wakati akicheza pale City, alikubali mkataba wa miaka miwili kujiunga na klabu hiyo ya Basque mapema mwezi huu.

Sociedad ilimaliza nafasi ya sita kwenye msimamo wa LaLiga msimu wa 2019-20, ingawa walishinda mechi mbili tu kati ya 11 baada ya ligi kurudi tena.

Na sasa Silva, anaona kwamba anatosha kuisaidia timu yake mpya kutoa changamoto kwa Barcelona na Real Madrid katika kuwania mataji kwenye misimu inayokuja.

“Kwa hakika nina hamasa kubwa kuanza hapa na kukutana na wachezaji wenzangu wapya,” alisema akiwaambia waandishi wa habari.

“Timu hii inacheza soka la kuvutia na nina matumaini nitaongeza kitu fulani hapa na kuwa na miaka mizuri ya kuvutia.

“Nina matarajio makubwa katika suala la soka nitacheza na nafikiri tunaweza kushindania taji.”

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# CITY YATANGAZA KUMTAKA MESSI

●●●Guardiola anaamini atasaidia kuimarisha kikosi chake na kutimiza ndoto za kunyakua...

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER City inatarajia kumpa mshambuliaji, Lionel Messi mkataba wa miaka miwili kama atakubali kutua klabuni hapo akitokea Barcelona.

Taarifa zilizoandikwa na gazeti la Cadena Ser zinasema, City wako tayari kumnasa Messi ili awasaidie kutimiza malengo yao ya muda mrefu ya kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Gazeti hilo hilo liliandika kuwa Mkurugenzi wa Soka wa City, Txiki Begiristain tayari ameshatua jijini Barcelona kwa ajili ya kufanikisha mchakato huo wa kumsajili Messi.

Nyota huyo anatarajiwa kuungana na kocha wake wa zamani wa Barcelona, Pep Guardiola ambaye anajipanga kuhakikisha anamnasa Messi, lakini bado kazi si rahisi kwa City katika mchakato huo wa kumsajili raia huyo wa Argentina.

Kama watafanikiwa kumsajili Messi, City itaweka wazi kipengele cha kumwongeza mkataba mpya badala ya muda wa sasa wa miaka miwili ambao wameuainisha.

Messi ameendelea kuwaacha katika sintofahamu Barcelona baada ya kushindwa kutokea katika mazoezi kwenye siku ya pili ya maandalizi ya msimu mpya akionekana anataka kuona anafanikisha mchakato wa kuondoka klabuni hapo.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 33 yuko huru kuondoka kama mkataba wake unavyoelekeza, lakini LaLiga imetoa taarifa kwamba bado Messi ni mchezaji halali wa Barcelona, hadi mkataba wake utakapomalizika ifikapo Juni 30, mwakani na klabu yoyote inayohitaji huduma yake italazimika kulipa ada ya pauni milioni 700.

Messi atakumbana na adhabu ya kulipa faini ya pauni milioni 1.1 na kusimamishwa baada ya kukosa mazoezi ya kwanza ya maandalizi ya kuelekea msimu mpya ambayo Barcelona wameanza.

Baba wa mshambuliaji huyo, Jorge anajiandaa kukutana na Bodi ya Wakurugenzi ya Barcelona wiki hii ili kufikia muafaka wa jambo hilo linaloendelea kati ya mwanawe na klabu.

Naye mgombea nafasi ya urais wa klabu hiyo, Toni Freixa amesisitiza Messi hawezi kubadilisha uamuzi alioutangaza na anaamini mshambuliaji huyo ataondoka klabuni hapo.

"Kutokana na taarifa mbalimbali nilizozipata, uamuzi uliofanywa na mchezaji huyo ambaye ni mkongwe hauwezi kubadilika. Messi ni mchezaji anayetaka kuona anapata mafanikio makubwa. Yeye peke yake hawezi kufikia mafanikio hayo makubwa, anahitaji kuona hilo linafanywa na timu nzima," alisema.

Klabu mbalimbali zimeweka wazi nia ya kumsajili Messi tangu alipotangaza uamuzi wa kuondoka Barca, ikiwamo PSG, Juventus na Manchester United.

## KWA UFUPI

**FREIXA: MESSI ANAONDOKA**

MSHAMBULIAJI Lionel Messi anatarajiwa kuondoka Barcelona katika kipindi cha majira ya joto na kama 'anaonekana' atahamia katika klabu ya Manchester City, mgombea urais, Toni Freixa, amesema. ***(Goal)***

**MESSI AITWA ARGENTINA**

RAIS wa Argentina, Alberto Fernandez, ameemtaka mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi kurejea katika klabu yake ya utotoni ya Newell's Old Boys. ***(Evening Standard)***

**HAVERTZ KUWEKA REKODI**

CHELSEA imekubali kumsajili kiungo wa Bayer Leverkusen na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Kai Havertz (21), kwa dau la pauni milioni 72 ambalo litaweka rekodi ndani ya klabu hiyo, na itafanya bajeti yao katika usajili wa majira ya joto kufikia pauni milioni 200. ***(Guardian)***

**UPAMECANO ANUKIA UNITED**

MANCHESTER United imeweka wazi inahitaji saini ya beki wa RB Leipzig Mfaransa, Dayot Upamecano, ambaye ana umri wa miaka 21. ***(ESPN)***

**LINGARD, PEREIRA KUUZWA**

MANCHESTER United inajiandaa kumuuza kiungo wa Timu ya Taifa ya England, Jesse Lingard (27), pamoja na kiungo wa Brazil, Andreas Pereira (24), ili kupata fedha za kugharamia maboresho kwenye klabu hiyo ya Old Trafford. ***(Mail)***

**CEBALLOS KUBAKIA ARSENAL**

KIUNGO wa Hispania, Dani Ceballos (24), hivi karibuni anatarajia kujiunga tena na kikosi cha Arsenal kwa mkopo wa muda mrefu akitokea Real Madrid. ***(Guardian)***

**WAARABU WAMTAKA OZIL**

KLABU mbalimbali za Saudi Arabia na Qatar zimeonyesha nia ya kumsajili Mjerumani, Mesut Ozil katika kipindi hiki cha majira ya joto, lakini kiungo huyo mchezeshaji wa Arsenal mwenye umri wa miaka 31, hana mpango wa kuondoka jijini London. ***(Telegraph)***

**SPURS, HART WATETA**

TOTTENHAM imeanza mazungumzo ya kusaini mkataba mpya na golikipa Mfaransa, Hugo Lloris (33), licha ya kumsajili, Joe Hart ambaye alikuwa mchezaji huru hivi karibuni wakati dirisha la usajili lilipofunguliwa. ***(Football Insider)***

**SPURS WAMTAKA KING**

MABOSI wa Spurs wako katika mazungumzo ya kumsajili straika wa Bournemouth na Timu ya Taifa ya Norway, Josh King na pia wanamhitaji mshambuliaji, Callum Wilson (28). ***(Talksport)***

**WILSON AGEUKA LULU**

ASTON Villa imeweka wazi inahitaji kupata saini ya mshambuliaji wa Bournemouth, Callum Wilson ambaye ana umri wa miaka 28 na anawindwa pia na Spurs. ***(Mail)***

**MARTINEZ ANUKIA SHALKE**

KLABU ya Schalke imetangaza kuanza mchakato wa kuwania saini ya golikipa wa Arsenal, Emiliano Martinez (27), ambaye ni raia wa Argentina na anawindwa pia na Aston Villa. ***(Sky Sports)***

**HOLDING KITAELEWEKA**

ARSENAL imekubali kumpeleka kwa mkopo beki wake wa kati, Rob Holding (24), katika klabu ya Newcastle United, mchakato ambao unatarajiwa kukamilika wiki hii. ***(Talksport)***

**RAKITIC KUTUA SEVILLA**

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Croatia, Ivan Rakitic (32), anajiandaa kuondoka Barcelona na kujiunga na Sevilla kwa ada ya kawaida. ***(Goal)***

## HABARI MICHEZO




Wachezaji wa Yanga wakiingia na bango la shukrani kwa wadhamini wao Kampuni ya SportPesa katika siku ya kilele cha Wiki ya Wananchi iliyofanyika Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa Mkapa jijini, Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# YANGA: USAJILI WETU WAFANYIKA KISASA

**Na Saada Akida**

BAADA ya kumpokea mshambuliaji, Yacuoba Sogne, kutoka Burkinafaso, uongozi wa Yanga umesema malengo yao ya usajili kuelekea msimu mpya wa 2020/21 yamekamilika kwa kiwango kikubwa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Uwekezaji wa Kampuni ya GSM, Hersi Saidi, alisema klabu imefanya usajili mzuri kwa wachezaji wa ndani na wa kigeni na kuweka wazi nafasi mbili za wachezaji wa kimataifa zilizobakia zitajazwa kwenye kipindi cha dirisha dogo la usajili.

Hersi alisema 'jicho' lao limewaona nyota wawili ambao wa Aigle Noir ambao ni Ndikumana Athumani na Koffi Kouasai, lakini wamejipanga kuwafuatilia zaidi na kufahamu ripoti ya nidhamu za wachezaji hao.

Alisema hawatawasajili haraka kwa kuepuka kurudia makosa ya msimu uliopita na hivyo wanahitaji kupata muda mrefu wa kujiridhisha na viwango vyao.

"Hao wachezaji tumewaona na hatuwezi kukurupuka kuwasajili, mchezaji kumwona mechi moja tu haitoshi, tunawafuatilia na endapo benchi litawahitaji kwa kipindi hicho basi tutawasajili," alisema Hersi.

Aliongeza kwa sasa wanaliachia benchi la ufundi ambalo linaloongozwa na Kocha Mkuu, Zlatko Krmpotic kukijenga kikosi kwa ajili ya kufanya vema kwenye msimu unaotarajiwa kuanza Jumapili.

"Malengo yetu makubwa ya kwanza yalikuwa ni kusajili vizuri na tayari tumekamilisha, jukumu lililokuwapo sasa ni kwa kocha kuandaa kikosi chake kufikia malengo yetu ya kutwaa ubingwa," alisema Hersi.

Naye Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema tayari kocha wao ameanza majukumu yake rasmi na timu inaendelea na mazoezi kwa ajili ya mechi dhidi ya Tanzania Prisons itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, jijini.

"Maandalizi yanaenda vizuri, wachezaji wote wameshaanza mazoezi akiwamo, Yacouba Sogne aliyetua jana (juzi), naye atakuwapo katika programu ya kocha inayotarajiwa kufanyika mara mbili kwa siku," alisema Bumbuli. Wakati huo huo, Ofisa Mhamasishaji wa klabu hiyo, Antonio Nugaz, alisema mwendelezo wa Wiki ya Mwananchi utaendelea hivi karibuni kwa kufanya uzinduzi wa duka la jezi litakalofunguliwa kwenye makao makuu ya klabu yao.

"Pia kuna Kubwa Kuliko ambayo harambee itakayopatikana tutaitumia kuanza safari yetu ya ujenzi wa kiwanja chetu cha Kigamboni ambacho tutakijenga kwa nguvu za wananchi," alisema Nugaz.

## Ngasa asajiliwa Ndanda, Kessy arejea Mtibwa

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI dirisha la usajili kuelekea msimu wa 2020/21, likifungwa rasmi juzi saa 5:59 usiku, aliyekuwa winga wa Yanga, Mrisho Ngasa ametangazwa kujiunga na Ndanda iliyoshuka daraja wakati beki wa Nkana FC ya Zambia, Hassan Kessy amerejea Mtibwa Sugar.

Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF), Clifford Ndimbo, alisema jana waliofanikiwa kusajiliwa ni wale waliofanikisha usajili kwenye muda sahihi.

"Dirisha limefungwa, wale waliofanikiwa kusajiliwa ni wale waliosajiliwa kwenye muda ulio sahihi, naamini klabu zimefanikiwa kukamilisha taratibu zote, sasa kama kuna jambo lingine limejitokeza baada ya kufungwa, basi taratibu kutoka kwenye taasisi zitafuata na tutaweza kuzungumza chochote," alisema Ndimbo.

Akizungumza na gazeti hili, Ofisa Habari wa Ndanda FC ya Mtwara, Idrisa Bandari, alisema wamekamilisha usajili wao kwa ajili ya msimu mpya na mmoja wa nyota waliofanikiwa kunasa saini yake ni Ngasa.

"Tumekamilisha usajili wa Ngasa, tunapokwenda kucheza Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara, tunahitaji wachezaji wakomavu na wenye uwezo ambao watatusaidia kupanda tena Ligi Kuu," alisema Bandari.

Aliwataja wachezaji wengine waliowasajili ni pamoja na Paul Ngalema na William Lucian 'Gallas'.

Mtandao rasmi wa Mtibwa Sugar unaonyesha wamefanikiwa kumnasa Kessy ambaye aliwahi kuzichezea Simba na Yanga, pamoja na Mfungaji Bora wa Ligi Kuu Zanzibar, Ibrahim Hamad Hilika kutoka Zimamoto kwa kumpa mkataba wa miaka miwili.

# Baobab watamba kuendeleza vipaji

**Na Mwandishi Wetu**

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi na Awali ya Babobab iliyopo Mapinga mjini Bagamoyo, 'wametia fora' kwenye bonanza kwa kuonyesha vipaji vya aina mbalimbali.

Katika bonanza hilo lililowashirikisha wanafunzi wa shule ya awali na msingi, wanafunzi hao walionyesha umahiri kwenye kuigiza michezo mbalimbali ikiwamo ile ya maonyesho ya mavazi.

Moja ya sanaa walizofanya vizuri wanafunzi hao ni onyesho la mitindo ya mavazi ambayo chipukizi hao walipita jukwaani wakiwa wanajiamini na kutangaza ubunifu wa nguo walizovaa.

Akizungumza na gazeti hili, Mkuu wa shule hiyo, Ireneus Njelekela, alisema waliandaa bonanza hilo kwa ajili ya kuendeleza vipaji vya wanafunzi wao kwenye fani mbalimbali.

Njelekela alisema mbali na masomo ya darasani, shule imeona umuhimu wa kuwakutanisha wanafunzi hao kwenye bonanza ili waonyeshe vipaji walivyonavyo katika sanaa ya mitindo ya mavazi, muziki wa bongo fleva na maonyesho ya mitindo ya mavazi.

Alisema watakuwa wakiandaa bonanza kama hilo kila miezi mitatu kwa ajili ya kuvumbua vipaji vipya kwa sababu wanaamini wakiviendeleza vitawanufaisha kwenye maisha yao ya baadaye.

"Mbali na masomo ya darasani tumeona kuna umuhimu wa kubaini vipaji vya wanafunzi na kuvikuza, mtoto lazima alelewe katika nyanja mbalimbali kwa sababu mwisho wa siku anaweza kuishi kwa kutegemea kipaji chake," alisema kiongozi huyo.

"Kuna mifano ya wanamuziki wengi ambao wamefanikiwa sana kwenye maisha kutokana na vipaji walivyonavyo, mwanafunzi anaweza asifanye vizuri sana darasani, lakini akawa na kipaji kitakachompa maisha mazuri sana," aliongeza.



Wanafunzi wa Shule ya Awali ya Baobab iliyoko Mapinga, Bagamoyo wakipita katika onyesho la mavazi kwenye bonanza lililofanyika shuleni kwao mwishoni mwa wiki iliyopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Michezo
Jumatano Septemba 2, 2020
Nipashe



## CITY YATANGAZA KUMTAKA MESSI

HABARI UK 22



Kiungo wa Simba, Saidi Ndemla (kulia), akipambana kuwania mpira dhidi ya mchezaji wa AFC katika mechi ya kirafiki iliyochezwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini, Arusha juzi. Simba ilishinda mabao 6-0. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YAPELEKA SHANGWE MBEYA

● ● ●Yapokewa kwa heshima jijini humo, Sven afunguka wako tayari kuendelea 'kuwakera'...

**Na Somoe Ng'itu**

KIKOSI cha mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba kiliwasili salama jijini Mbeya jana mchana na Kocha Mkuu wa timu hiyo, Sven Vandenbroeck, amesema wanatarajia kuanza msimu mpya wa ligi kwa ushindi kama ilivyokuwa katika mechi ya ufunguzi ya Ngao ya Jamii.

Simba inatarajia kufungua pazia la msimu wa 2020/21 Jumapili kwa kuvaana na timu mpya iliyopanda daraja ya Ihefu FC kwenye Uwanja wa Sokoine jijini humo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Sven alisema hakuna mechi rahisi kwenye Ligi Kuu kwa sababu ya ubora wa vikosi vilivyosajiliwa na kila timu inajipanga kufanya vizuri kwenye michezo ya awali.

Sven alisema wanaamini timu itakayopata ushindi katika mechi zake za kwanza, ndiyo itajiweka kwenye mazingira mazuri kwenye mbio za ubingwa na wachezaji wake watakuwa kwenye nafasi nzuri ya kupambana.

Kocha huyo alisema licha ya kikosi chake kuwa na nyota wenye uwezo, hakuna mchezaji ambaye ana namba ya kudumu katika kikosi cha kwanza, hivyo nyota wote watalazimika kujituma ili kupata nafasi ya kucheza.

"Tutaelekea kwenye mechi ya ligi, tuko tayari, tunajua hakuna mechi rahisi mbele yetu, sisi ndio mabingwa wa msimu uliopita, tunatakiwa kuendeleza ubora wetu, tunahitaji kujiimarisha kila siku," alisema Sven.

Kocha huyo aliongeza wanakwenda kukutana na timu mpya, hivyo watatumia muda kiasi kuwasoma wapinzani wao na baada ya hapo watacheza kwa kasi ili kutimiza malengo ya kuvuna pointi tatu muhimu.

Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, aliliambia gazeti hili kikosi chao kilipokelewa na mashabiki na wanachama wa timu hiyo ambao kila mmoja alionekana kufurahi kuwaona nyota wa timu hiyo.

Rweyemamu alisema jana jioni walitarajia kufanya mazoezi mepesi na leo asubuhi wataanza programu maalumu kuelekea mchezo huo dhidi ya Ihefu.

"Tunatarajia kufanya mazoezi kwenye Uwanja wa Sokoine, huenda tukawa na vipindi viwili kwa siku au kimoja, kesho (leo) asubuhi tutakabidhiwa na kocha mkuu, kwa kifupi timu iko tayari kwa mapambano, kila mechi kwetu ni muhimu, hatutadharau mchezo wowote," Rweyemamu alisema.

Simba itashuka uwanjani Jumapili ikiwa na kumbukumbu ya ushindi mnono wa mabao 6-0 walioupata kwenye tamasha la Simba Day dhidi ya Vital'O kutoka Burundi, huku pia ikichukua Ngao ya Jamii baada ya kuwafunga Namungo FC magoli 2-0 Jumapili iliyopita jijini, Arusha.

## ZLATKO ATAMBA YANGA ITATIKISA

**Na Faustine Feliciane**

HUKU zikiwa zimebakia siku nne kabla ya kuanza kwa msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2020/21, Kocha mpya wa Yanga, Zlatko Krmpotic, amesema anatamani kucheza mechi moja ya kirafiki, lakini akakiri muda uliobakia ni mchache, imefahamika.

Zlatko alikiongoza kikosi cha Yanga katika mazoezi yaliyofanyika jana kwenye Uwanja wa Chuo cha Sheria kilichoko jijini Dar es Salaam akiwa na wachezaji wake wote waliosajiliwa akiwamo mshambuliaji mpya kutoka Burkinafaso, Yacouba Sogne, ambaye aliwasili nchini juzi.

Kocha huyo alisema wachezaji wake wamefanya mazoezi vema, lakini anasikitika kukosa muda wa kucheza mechi ya kirafiki ili kuwaimarisha kabla ya kuanza msimu mpya.

"Ingekuwa vema kama tungepata mchezo wa kirafiki, lakini muda ni mfupi kabla ya kuanza kwa ligi, tunaendelea na maandalizi na naamini mambo yataenda katika mstari tunaoutaka," alisema Zlatko.

Aliongeza kama angepata muda wa wiki mbili au tatu, angepata muda wa kufanya majaribio ambayo yangewaimarisha wachezaji wake na kupata kikosi imara zaidi kitakachokuwa tayari kupambana.

"Kuna programu ya mazoezi nimeiandaa, tutaitumia kwa kipindi hiki kilichobakia ili kuweka muunganiko mzuri kwa wachezaji," Zlatko alisema.

Meneja wa timu hiyo, Hafidh Saleh, alisema anaamini kikosi chao kitaanza vema msimu mpya baada ya kila mchezaji kuwa na kiu ya mafanikio.

"Tuko tayari kwa msimu, ingawa Kocha Zlatko aligusia kupata mchezo wa kirafiki baada ya ule wa Jumapili dhidi ya Eagle Noir, lakini muda umekuwa mfupi," alisema Saleh.

Yanga itaanza kampeni ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kuwakaribisha 'Maafande' wa Jeshi la Magereza, Tanzania Prisons Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamini Mkapa jijini.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >